# *Kweli Zisizoshindwa Za Mungu Aliye Hai*

. . . Breeding, Kentucky; lazima niwe kule saa mbili kwa ajili ya ibada ya mazishi, kuzika . . . Henry Branham, ambaye ni binamu yangu, mkewe alikufa. Na ombi lake la mwisho, kwamba niongoze ibada ya mazishi yake. Na hiyo ni huko Breeding, Kentucky. Hiyo ni karibu maili mia moja hamsini au sitini, nadhani, huko chini, au kitu kama hicho, huko kusini. Na nitalazimika kuondoka mapema kidogo, kwa sababu ya kufika huko.

2 Halafu turudi basi usiku wa leo, na kuondoka kesho alasiri. Sisi ni . . . Ninatakiwa kuwa huko Tulsa kwa ajili ya juma lijalo, huko Tulsa, Oklahoma. Lakini sitapata kwenda kabla ya Jumanne, kwenda Tulsa. Halafu turudi Jumamosi usiku, tuwe humu ifikapo Jumamosi usiku.

3 Na kisha Jumapili asubuhi, Jumapili ijayo asubuhi, yapata saa tisa, tuondoke kuelekea Magharibi, halafu hatutarudi tena mpaka msimu huu wa majani kupukutika, nitakaporudi na kuichukua familia yangu na kadhalika; nasi tutarudi wakati mwingine msimu huu wa majani kupukutika, Bwana akipenda. Na bila shaka nataka kuliomba kanisa liniombee.

4 Nami nilitaka kupata kuona ikiwa ningeweza kuwa humu. Hebu tuone, huu hautakuwa ndio usiku wa ushirika, ama vipi? [Ndugu Neville anasema, "Hapana."—Mh.] Hapana. Nilikuwa hapa usiku wa mwisho wa ushirika. Lakini sikurudi kwa ajili ya . . . Sitaweza kuwa hapa kwenye wakati wa huu ushirika. Itakuwa Jumapili ijayo usiku, ["Naam."] itakuwa ushirika? Daima napenda kuuhudhuria huo, unaona. Daima, mlapo na kuinywa hii, mnaonyesha kifo cha Bwana hata atakapokuja tena.

5 [Ndugu Neville anasema,"Ndugu Branham?"—Mh.] Naam. ["Naomba utangaze kwamba, siku ya kuzaliwa ya Dada Edith, tutakuwa na kusanyiko dogo kule Ijumaa ijayo usiku."] Vema, hilo ni zuri sana. Dada Edith Wright amekuwa siku moja mdogo zaidi. Naye . . . Watakuwa na kusanyiko dogo nyumbani kwake Ijumaa ijayo usiku. Vema, ni zuri jinsi gani! Vema. Je, umma umealikwa? ["Mtu yeyote."] Umma umealikwa kwenye siku ya kuzaliwa ya Dada Edith ya . . . Atakuwa na yapata miaka kumi na minane; hiyo ni kweli, Dada Edith?

6 Ni kama vile nilivyosema hivi majuzi, nilisema, "Mnajua, ndiyo kwanza nipite ishirini na mitano."

Ndipo jamaa fulani akaangalia pande zote, akasema, "Ati?"

7 Nami nikasema, “Mara yangu ya pili.”

8 [Dada mmoja anasema, “Ndugu Branham.”—Mh.] Lini? [“Thelathini na tisa.”] Atakuwa na thelathini na tisa. Jamani, hiyo haionekani inawezekana, sivyo? Thelathini na tisa. Daima mimi humtaja kama msichana mdogo tu, unajua, kwa sababu wakati nilipomjua Edith kwa mara ya kwanza, nadhani hiyo ni . . . Edith, hebu tuone, nimekujua, nadhani, kama miaka ishirini na kitu sasa, nadhani, miaka ishirini na mitano, labda ishirini na minane.

9 Mnaona, nimekuwa nikihubiri yapata miaka thelathini na mmoja, nadhani, kwa hivyo nadhani niliwajua mara tu baada ya kuanza kuhubiri, familia ya Wright. Kwa hivyo, basi nashukuru sana kwamba niliwajua watu hao. Bila shaka wamekuwa uvuvio maishani mwangu.

10 Na kama ikibidi familia ya Wright kupita iingie katika Umilele, nami nilikuwa bado ningali hai, nisingeweza kupita mahali hapo bila kuvua kofia yangu, kuwazia juu ya mambo makuu ambayo Mungu amefanya kwenye ubavu wa kilima kile pale! Loo, jamani! Hapo ndipo, loo, kila kitu kikitendeka huko chini. Nami nimeona huko, yakitukia, Malaika wa Bwana akifanya ziara kwa ajili ya Georgie Carter. Kuchukua mahali ambapo Yeye aliniongoza kwenye ubavu wa kilima usiku huo, pamoja na ule mmea tambaaji wenye sumu. Halafu Yeye akakutana nami kule pia katika ono, na akaangaza chini kutoka kwenye vichaka-mbwa. Wao . . . Loo, jamani, ni mambo mengi sana yametukia.

11 Ndugu Wright akiwa karibu na kufa, wakati madaktari wote walikuwa wamepitia. Na washiriki wa kanisa lake kule chini, wakimwambia, “Nenda kamwite mponyaji wako wa Kiungu sasa.”

12 Mimi nikiwa nimeketi juu ya kilima, nikilia kwa siku nne, nikimwombea. Bwana akanena ono, akasema, “Nenda kamwambie BWANA ASEMA HIVI. Atamzika yule jamaa anayemdhihaki.” Na alimzika. Hiyo ni kweli. Na mambo yote hayo.

13 Na kisha hapo ambapo Roho Mtakatifu, kwa mara ya kwanza katika historia ya—ya Kanisa, ambapo niliwahi kuona likitukia, wakati Yeye alipokuwa amenena na . . . kuchakulo hao wakaweko. Pia, akampa Dada Hattie chochote ambacho alitaka kuomba, haidhuru ni nini, pesa au kitu chochote kile, kasema, “Kitawekwa mkononi mwako hivi sasa.” Aliomba nafsi za wavulana wake wawili. Naye Mungu akampa. Na mambo mengi sana yametukia kule chini kilimani. Mungu awabariki, ndilo ombi langu.

14 Aisee, mtoto Sharon Rose anaumwa hapa, mtoto Sharon Rose Daulton. Sharon Rose yuko wapi? Hivi . . . Ametoka nje sasa hivi. Uh-huh. Sawa, tunaenda . . .

15 [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Wasemaje? [Huyo ndugu anazungumza tena.] Vema, unajua nini, hebu tuwaombee sasa.

16 Sababu, nitawaambia kinachonipasa kufanya. Mara tu ninapoweza kumalizia, ninataka kufika, lazima nifike huko Kentucky. Nami nina . . . Vema, kama ni maili mia na hamsini, sijui. Ni Breeding, Kentucky. Sina fununu ni umbali gani. Unakwenda mpaka njia ya kugeukia, halafu yapata umbali uo huo, au mbali zaidi kidogo tena, unaendelea mbele, huko chini kupitia kwa Ndugu Beeler, na kuendelea kupitia kwenye mji huo, na mji mwingine, na mji mwingine, na mji mwingine, kufikia kanisa dogo alilojenga babu yangu, kanisa dogo la Kimethodisti ambalo nilihubiri miaka ishirini na mitano, thelathini iliyopita.

17 Na mama huyu atazikwa kutoka huko. Alikuwa muuguzi. Naye alikufa ghafla, na ombi lake la mwisho lilikuwa—lilikuwa kwamba nihubiri mazishi yake. Halafu tena baadhi ya watu wangu walikuja huku jana na kuuliza ikiwa ningeenda kuihubiri, nami—nami kamwe nisingeweza kuwakatalia; yeye akiwa ameketi hapo akilia, akisema, "Ni ombi lake la mwisho." Kwa hiyo ilikuwa ni vigumu, mwajua. Basi nikasema tu, "Vema, ninataka kushuka kwenda kanisani, nami ninataka kuona jamaa huko, na kisha niichukue hiyo, pia." Kwa hivyo, kwa namna fulani sina budi kuharakisha ili kuipata, kwa hiyo mnaelewa.

18 Sasa wakati wakiwapata, ninaamini, Ndugu Daulton . . . [Ndugu mmoja anasema, "Ameenda msalani."—Mh.] Loo, vema, hiyo ni sawa. Hiyo ni ninii tu, tutangoja kidogo tu hata . . .

19 Umlete mtoto Janice hapa. Na mtu mwingine yeyote anayetaka kuja kuombewa, hiyo ni sawa. Na sisi tuna . . .

20 Habari yako, Janice? Jamani, huyu hapa—huyu hapa mama mzuri. Njoo hapa. Sababu ya kuwa mrembo sana, huyu ni mtoto wa dada yangu. Nami nataka kurudi *hapa* ili watu waweze kunisikia, ninachosema. Sasa, maskini kipenzi huyu, ana mama mwenye afya na baba mwenye afya, lakini kuna jambo lililompata mtoto huyu. Yeye ni dhaifu, dhaifu sana, na mdogo na mwembamba. Wa kupendeza awezavyo kuwa; na, kwa kweli, mnajua ningewazia hivyo. Lakini siku zote mtoto huyu ana shida. Shetani anajaribu kumchukua huyu mtoto. Na labda Mungu ameweka mkono Wake juu ya huyu mtoto, mnaona. Tunaweza kutazama, unapoona Shetani akifanya kazi. Hiyo ni ninii tu, angalieni, kuna kitu fulani kimelala pale mahali fulani. Sasa amekuwa mgonjwa kwa siku chache.

21 Sikuenda huko nje, kwa sababu sikujua kama alikuwa amepona au la. Ilinibidi kwenda Florida na kwingine huko.

22 Na, lakini homa ikaongezeka. Sivyo, dada? Yeye, alishikwa na homa kali sana, na yapata mia moja na . . . [Dada mmoja anasema, "Tatu."—Mh.] mia moja na tatu, hiyo inafanya digrii

tano za homa. Madaktari hawajui ni nini. Nao kwa namna fulani wanafikiri ni homa ya baridi yabisi. Ikiwa ingekuwa homa ya baridi yabisi, hiyo inaweza kuuacha moyo wake katika hali mbaya sana, kama ile iliyomwua mjomba wake. Lakini nitaudai uhai wa mtoto huyu kwa ajili ya Yesu Kristo, mnaona.

23 Nanyi mwajua Daudi, kama vile nimesema hapo awali, hapa. Daudi akamwambia Sauli, akasema . . . Sauli alitaka kumpa vazi la kujihami pamoja na mkuki, ili apigane na Goliathi, lile jitu. Akasema, “Mimi—mimi—mimi sijui chochote juu ya vitu hivyo,” akasema, “lakini hebu nichukue kombeo hili, kile ambacho nimethibitisha, unaona.” Akasema, “Simba akija, akamchukua mmoja wa kondoo wa baba yangu. Nami nikamfuatilia, pamoja na kombeo hili, na nikampata. Nikamrudisha kondoo.”

24 Sasa, hawa ni kondoo, pia, wana-kondoo na kondoo, kondoo wa Mungu. Sasa hebu tukawafuatilie asubuhi ya leo, kama Kanisa la Mungu, tupate kuwarudisha. Sasa daktari hajui amfanyie nini huyu mtoto.

25 Na mimi nadhani msichana mdogo wa Ndugu Ed, pia, ameshikwa na namna fulani ya ugonjwa wa pumu au kitu fulani.

26 Naam, ninaamini kwamba Yesu alisema hivi, “Nakupa funguo za Ufalme. Lolote utakalofunga duniani, litafungwa Mbinguni. Utakalofungua duniani, litafunguliwa Mbinguni.” Tunaamini hilo, kwa moyo wetu wote. Sasa, Mungu atupe imani ya kuliamini kwa moyo wetu wote, tunapoomba.

27 Baba yetu wa Mbinguni, ninashikilia hapa ua hili dogo dhaifu la familia ya Weber, zuri, jororo, dhaifu. Nao matabibu, wao ni waaminifu; wanajaribu kwa yote wajuayo, kujaribu kujua shida ya mtoto ni nini, lakini hawawezi kuijua. Basi ninaushika mkono wake, wala siamini ana homa yoyote ya baridi yabisi. Ninaamini, kama alikuwa nayo, Wewe ungeniambia. Ninaamini ni Shetani akijaribu kuyavuruga maisha ya mtoto huyu. Nasi tunamdai asubuhi ya leo, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

28 Ewe adui wa maisha ya mwanadamu, ewe adui wa Mungu Mwenyezi, naja kwa niaba ya mtoto huyu, kukutoa kwake. Katika Jina la Yesu Kristo, mwache mtoto huyu mdogo. Huenda ukaweza kumkwepa daktari, lakini huwezi kumkwepa Mungu. Maombi haya ya imani yamelengwa, katika Jina la Bwana Yesu, yapate kukupiga katika mwili wa mtoto huyu. Nayo yatapiga sehemu hiyo muhimu popote ulipojificha, nawe utafichuliwa na kutolewa nje. Naye huyu mtoto ataishi na kuwa mzima, kwa maana tunamkabidhi katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

29 Delores, nisingehofia chembe moja zaidi juu yake. Naam. Janice atakuwa mzima, na hakuna lingine.

30 Halafu tuna mtoto Daulton hapa. Hawa si ni wapendwa! Ni maskini mtoto mzuri jinsi gani! Jamani, wewe ni mzito

sana! Je, huyo si ni mtoto mpendwa, msichana mdogo kweli anayeonekana Muairishi mwenye macho ya samawati na nywele nyeusi. Naye anapumua kwa shida, mapafu yake madogo na kila kitu. Aliambukizwa na kitu kama pumu, kama, kwenye koo lake.

31 Ee Bwana, simba na dubu waliingia, akasema Daudi, na kuchukua baadhi ya wana-kondoo wa baba, naye akawafuatilia, na aliweza kumshinda simba huyo na huyo dubu. Nasi tunakuja asubuhi ya leo kama waaminio (kama vile Daudi alivyokuwa) katika Mungu wa Mbinguni, Yule aliyeziumba Mbingu na nchi, twaja kwa ajili ya mtoto huyu, katika Jina la Yesu Kristo.

32 Nawe, Shetani, wewe ambaye umemtesa mtoto huyu, itakubidi umwachilie, kwa maana tunakuamuru umwachilie huyu mtoto, apate kuwa mzima. Ninakukemea, Shetani, na kukuamuru kwa ufufuo wa Yesu Kristo Mwana wa Mungu, ambaye alipata ushindi juu yako, na nguvu zako zote zikaharibiwa. Basi huna nguvu. Nami ninapata ushindi juu yako, kwa imani katika Jina la Yesu Kristo, ambaye ni Mwana wa Mungu, ambaye alituamuru kwa Injili hii, kwamba katika Jina Lake tunapaswa kukutoa; ni agizo lililotolewa na Kristo. Utamuacha. Kwa maana, tunakuamuru, katika Jina la Yesu Kristo, kumwacha huyu mtoto. Naye atakuwa mzima.

33 Sasa usiwe na shaka hata kidogo, Dada Daulton. Usihofu tena. Mungu alisema hivyo, hilo latosha.

34 Huyu jamaa mdogo ni nani? [Dada mmoja anasema, "Lisa Wilson. Ana uvimbe."—Mh.] Loo, uvimbe juu ya jicho lake. Sasa karibu yeye ni mwanamke mchanga, sijui kama ninaweza kumwinua au la. Lakini yeye ni mrembo sana. Anaitwa Wilson. Lela, Lela? ["Lisa."] Lisa Wilson. Si yeye ni maskini mtoto mrembo? Ana uvimbe juu ya jicho lake. Vema, Yesu huponya vivimbe, sivyo? Itambidi kuninii...?...["Sio wa kufisha."] Vema, ni—ni uvimbe mdogo tu wa mafuta, umelegea, hauna mizizi yoyote...?...Na tuombe.

35 Ee Bwana, tunamleta maskini huyu kipenzi Kwako, katika Jina la Bwana Yesu, na kumshikilia, kama mtoto asiye na hatia, Mbele za Mungu. Naye ibilisi amemfanyia uovu huu, na angelipofusha jicho lake, kwake, kama angeweza, lakini Wewe umemshinda nguvu hata na zaidi.

36 Tunakuamuru, Shetani, kwa Jina la Yesu Kristo, Yule aliyepata ushindi juu yako pamoja na mateso yote unayowapa watu. Tunakuamuru, kwa Jina Lake, kwa agizo lililotolewa na Malaika aliyetumwa kutoka kwa Mungu, kwamba umwache mtoto huyu, naye anapona, kwa Jina la Yesu Kristo. Amina.

37 Ubarikiwe mtoto Lisa. Nisingekuwa na shaka hata kidogo, tena. Amini tu itakuwa vema.

38 Vema, Dada Bruce. Sasa wewe, ukitaka, wanawake hawa waliosimama hapa, Joyce, sogea karibu kidogo tu hapa, watu

waweze kuingia. Ndugu Neville, njoo, tafadhali, ukawapake mafuta.

[Dada anasema, "Ningependa kusimama mahali pa binti yangu."—Mh.] Mahali pa binti yako. ["Msichana *huyo* anasimama mahali pa mpwa wangu."] Mahali pa mpwa wako. Mpwa wako; binti.

Na wako ni nani, dada? [Dada anasema, "Mwanangu, . . .?. . .kukabidhiwa Mungu." Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

39 . . .kauli hizi zinajulikana kwa watu. Kwa kweli, dada yetu *hapa* ni kiwete, naona hilo. Ni yabisi kavu, sivyo, dada? [Ndugu mmoja anasema, "Nyonga iliyovunjika, naye akapata kiharusi."—Mh.] Nyonga iliyovunjika, kisha akapata kiharusi.

40 Mama huyu hapa ana shinikizo nyuma ya kichwa chake, kama mkono wa mtu unaokisukuma.

41 Dada Bruce ameumia mguu, naye pia ni . . .[Dada Bruce anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Bado yuko hospitalini. ["Nimeruhusiwa kuondoka . . .?. . . "] Ulianguka au nini? ["Nilianguka kutoka kwenye eskaleta . . .?. . . "] Huyo ni mmoja wa dada zetu hapa kanisani. Alianguka kutoka kwa eskaleta, na kweli yuko hospitalini. Umevunjika? [Dada Bruce anajibu.] Loo, ukano na mishipa ya damu, na kadhalika. Halafu, amesimama kwa niaba ya wengine, wapendwa wengine.

42 Nao wanawake hawa watatu hapa wamesimama kwa niaba ya wapendwa, tupate kujua sasa wakati tukiomba. Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu, kila mtu.

43 Ee Bwana Yesu, haja hizi zimefanywa kujulikana. Nayo Biblia imesema, "Haja yako na ijulikane katika kusanyiko la watakatifu." Hapa kuna wale ambao wanawaombea wapendwa, ambao wengine ni mahututi, wengine wamerukwa na akili, wakikana kwamba kuna Mungu aliye hai, na, magonjwa mengine. Kuna dada yetu hapa mwenye mguu uliovunjika katika hali mbaya, ametoka tu hospitalini hapa, asubuhi ya leo. Dada aliye na shinikizo kubwa nyuma ya kichwa chake. Na dada aliyevunjika nyonga na kiharusi. Wote wako hapa, Bwana. Wanawasilisha haja zao, na wamesimama mbele ya madhabahu ya Mungu; huku mafuta ya kupaka yaking'aa vichwani mwao, yanawakilisha Roho Mtakatifu. Nimesimama katika urahisi wa maarifa niliyo nayo ya Yesu Kristo na Neno Lake, na ninamwombea kila mmoja wao.

44 Mungu, ninapoweka mikono yangu juu yao, na wajibiwe maombi yao. Utujalie, Ee Mungu, katika Jina la Yesu. Na iwe hivyo, Baba, kwa Dada yetu Gertie, katika Jina la Yesu. Pia kwa Dada Bruce, Bwana, na iwe hivyo, haja yake, goti lake na viungo vyake. Kwa dada yetu mwenye maumivu nyuma ya kichwa chake; na iwe hivyo, Bwana, katika Jina la Yesu, naye ataokolewa kutoka kwenye hiyo. Shetani na aiondoe mikono

yake nyuma ya shingo yake. Lijalie. Naye dada yetu ambaye ni kiwete, alishikwa na kiharusi, na ana nyonga iliyovunjika.

45 Bwana, baadhi ya haya huenda yakaonekana ni madogo sana, na baadhi yao makubwa sana, lakini hakuna hata moja yao lililo dogo kupita kiasi wala hakuna lililo kubwa kupita kiasi Kwako. Wewe ni Mungu, juu ya yote. Nami ninaomba na kuwakomboa kwa maombi ya imani, kila mmoja wao; Bwana, kama mtumishi Wako, kuvunja nguvu za—za shaka au chochote kilicho juu yao. Ninawakabidhi ukombozi wao, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia kila mmoja apokee hasa kile alichoomba. Na kama kanisa hili, kitengo cha Mwili Wako, katika maombi sasa, tunawakomboa katika Jina la Yesu Kristo. Na waupokee sasa, kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

46 Mungu awabariki kila mmoja, sasa upokeeni. Nendeni, mkapokee uponyaji wenu na baraka.

47 Sasa hapana shaka akilini mwetu. Sivyo? Hata shaka moja. Mungu atalitenda? Mnaiamini, kila mtu? Mungu atayatimiza. Kila. . . Hataacha lolote bila kufanywa, Yeye atafanya lile hasa tulilomwomba kufanya. Maana, Yeye hawezi kufanya lingine lolote na kubaki Mungu, mnaona. Ikiwa hatuna shaka, atatupatia.

48 Sasa msisahau kumwombea mtu ambaye kweli anahitaji maombi. Nyote mnajua huyo ni nani? Ni mimi. Naam, mimi ndiye ninahitaji maombi. Nikisimama kwenye pengo sasa, na kuendelea na safu ndefu ya mikutano, kote kupitia California, Oregon, Washington, na kuzunguka Oklahoma na maeneo tofauti. Watu watatoka Canada, na kadhalika. Nami sina budi kusimama kwenye pengo, kukiweko na tofauti za wahudumu na maoni, na nguvu za ibilisi; nao mwisho, wakati wa mwisho unakaribia.

49 Basi mtu fulani tu alisema hivi majuzi, akaja nyumbani kwangu. Ilikuwa ni ma—mama fulani, aliyeruka kwa ndege kutoka Ujerumani, na mtu mwingine akaja kutoka mahali fulani-fulani, wakasema Bwana aliwaambia waje, nao, *hivi, vile, vinginevyo*. Ndipo mtu mmoja akavuka barabara, akasema, "Je, unastahimilije?" Mnaona?

Nikasema, "Loo, ni neema Yake." Amina.

50 Ndipo ilinibidi kuruka kwenye ndege, kuruka usiku kucha kwenda California ama Arizona, ama, Florida. Nikarudi, ndipo nikaingia katika dhoruba. Ibilisi alijaribu kutuangusha, mnajua. Naye Bwana akatuleta humu. Halafu kesho yake asubuhi, jana, nilipaswa kuondoka kwenda Bakersfield, California, kwa dharura ya mhudumu fulani. Na ilininii tu. . . kamwe nisingeweza kufanya hivyo, ni hayo tu. Na, unaona, halafu unafika kwa *wengine,* nawe—nawe hujui uende wapi kutoka hapo, unaona. Ni, hapa kuna *huyu, huyu, huyu, huyu, huyu,* mnajua ninalomaanisha; na, basi, ni yupi? Na inawaudhi

wengine usipofanya hivyo, usipowaona wote, mnaona. Wala huwezi kuwaona wote. Kwa hivyo inakubidi tu kungojea na, jinsi unavyojisikia kuongozwa, ndipo unaenda tu.

51 Nilitaka kutoa pongezi nzuri ya mchungaji wetu. Hospitalini, jana usiku, kwa dharura, nilijivunia Ndugu Wood na Charlie na wengineo, ilikuwa ni usiku sana. Mama fulani aliyekuwa amelala, akifa, dada zake na hao wengine walikuwa pale. Naye alikuwa amepoteza fahamu kwa muda, akaamka na kumpokea Bwana Yesu. Nilipata kumwongoza mtu mwingine kwa Bwana Yesu, kule chini Florida, mwenye dhambi. Na majira yote ya usiku, na kila kitu, kwenye dharura, ina—inakupasa kumfuata mhudumu wakati mwingine upate kujua. Nami nikasikia matamshi mazuri sana hospitalini, juu ya mchungaji wetu wakati anapokuja kule, jinsi anavyowatembelea watu na kuwaombea wagonjwa, na ni mwaminifu kwenye wajibu wake. Ni—ninathamini hilo sana, kuwa naye juu ya kundi hili dogo, mtumishi wa Bwana, ambaye ni mwaminifu katika wajibu wake. Hamthamini. . . Mnamthamini, hakika mnamthamini, lakini sisi. . . Kuna njia fulani tu tunaweza kulionyesha zaidi, mnaona, kwa mtumishi mwaminifu wa Bwana.

52 Mtu fulani aliniuliza si muda mrefu uliopita, huko Chautauqua, mkutano wetu wa mwisho, "Ndugu Branham, unaendeleaje namna hiyo?"

53 Nikasema, "Huyu hapa Gene Goad, Pat Tyler, na kundi zima lao kama hawa jamaa hapa, ninapokuwa katika moja ya mikutano hiyo; wanalala kifudifudi, na kufunga kwa siku kadhaa wala hata hawali, nao wanaomba na kila kitu, kwa ajili yangu." Hayo ndiyo yanayoniendesha. Mnaona? Huo ndio uweza. Msaada wao unatoka kwa Bwana. Ndugu Daulton, loo, wengi wao tu, wa marafiki ambao hufunga tu na kuomba, kukataa chakula chao na kadhalika, na kufunga na, kuomba.

54 Sasa ikiwa Ndugu Gene, huko nyuma, yuko tayari kurekodi, sasa nitaninii. Ndugu Neville ataendelea na ibada baada tu ya kitambo kidogo. Ninataka kuongea kwa muda kidogo tu.

55 Na sasa ikiwezekana ninaweza kurudi, Edith, mpendwa, nasikia karamu yako ya siku ya kuzaliwa ni Ijumaa usiku; iwapo ninaweza kurudi kutoka Oklahoma kwa wakati mzuri, nitakuwa huku, unaona, Ijumaa usiku, iwapo naweza.

56 Na sasa wakati tukienda, nyote mtuombee. Na i—imesemwa katika Biblia, "Bwana nilinde mimi pamoja nanyi, mnaona, wakati tukiachana." Na afanye hivyo, na awalinde na kuwabariki, na anilinde na kunibariki, na atusaidie sote kuishi vyema sana tuwezavyo kwa utumishi Wake, mpaka tutakapokutana tena. Nami nitategemea maombi yenu wakati nikiwa nje hudumani huko ng'ambo, kukabiliana na adui. Kwa hivyo, mtuombee. Ninyi nyote ndugu wahudumu, Ndugu Humes

na Ndugu Beeler, na wengine wengi wenu hapa, niombeeni tu. Mnaelewa.

57 Sasa tunataka kufungua katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu, mlango wa 4. Nami nataka kuzungumza asubuhi ya leo, Bwana akipenda, juu ya somo liitwalo: *Kweli Zisizoshindwa Za Mungu Aliye Hai.*

58 Nataka kusoma kutoka kwenye kifungu cha 14, vyote pamoja na cha 23, cha Yohana Mtakatifu mlango wa 4. Tunaingilia mazungumzo sasa, ya Yesu akiongea na yule mwanamke kisimani. Yohana Mtakatifu, mlango wa 4, kifungu cha 14, pamoja na cha 23.

> *Lakini kila mtu anywaye maji nitakayompa mimi hataona kiu kamwe; lakini maji nitakayompa yatakuwa ndani yake kisima cha maji, yakibubujikia* hata *uzima wa milele.*

59 Sasa neno hapo kweli sio *daima*, utaona alama kidogo juu yake ikiwa liko katika, ikiwa una Biblia ya King James. Katika ya asili, inasema, "hata Uzima wa Milele." *Daima* ni kwa muda tu. *Milele* ni isiyo na mwisho.

> . . .*yakibubujikia* hata Uzima wa Milele.
>
> *Yule mwanamke* alimwambia, *Bwana, unipe maji hayo, nisione kiu, wala nisije hapa kuteka.*
>
> *Yesu akamwambia, Nenda kamwite mumeo uje naye hapa.*
>
> *Yule mwanamke akajibu akasema, Sina mume. Yesu akamwambia, Umesema vema, sina mume:*
>
> *Kwa maana umekuwa na waume watano; naye uliye naye sasa siye mume wako: hapo umesema vema.*
>
> *Yule mwanamke akamwambia, Bwana, naona ya kuwa u nabii.*
>
> *Baba zetu waliabudu katika mlima huu; nanyi husema ya kwamba huko Yerusalemu ni mahali patupasapo kuabudia.*
>
> *Yesu akamwambia, Mama, unisadiki, saa inakuja, ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala kule Yerusalemu.*
>
> *Ninyi mnaabudu msichokijua: sisi tunaabudu tukijuacho: kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi.*
>
> *Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli: kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu.*

60 Katika siku za Yesu wa Nazareti, wakati alipokuwa hapa duniani, akitembea katika mwili, Aliwakuta watu, katika siku Zake, wakitafuta dini ambayo ingewaletea ukombozi. Walitaka dini ambayo ingewakomboa kutoka kwa maovu yao yote na adui

zao. Na Ukristo ulikidhi kila changamoto ambayo waliomba. Ukristo ulikidhi mahitaji yao yote, na kila kitu walichoomba. Ulitoa changamoto kwa kila moja la mahitaji yao, lakini wasingeupokea.

61 Na ni karibu kama ilivyo siku hizi. Tunawaona watu siku hizi, kama ilivyokuwa wakati huo, wakitafuta dini ambayo itawafanyia kitu fulani, ambayo ita—ambayo itawaletea uhalisi fulani. Nao Ukristo halisi wa kweli hukidhi kila moja ya changamoto hizo, ila hawataupokea. Kamwe hawautaki. Tabia ya watu siku hizi. Siongei juu ya Kanisa lililozaliwa mara ya pili. Ninazungumza juu ya taifa na nchi, kwa jumla. Inaonekana hawautaki.

62 Ukitaka chochote, huwezi kupumzika mpaka ukipate. Yesu alisema, katika zile heri, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa maana watashibishwa." Ikiwa wana njaa na kiu!

63 Lakini siku hizi tunajaribu kuwapa watu kitu ambacho wanahitaji sana, nao hawataki kukikubali. Kamwe hawakitaki. Nao mtazamo wa watu haujabadilika. Na hata hivyo hiyo ndiyo hasa ulimwengu unahitaji siku hizi, ni dini ya Yesu Kristo, ukombozi kutoka kwa vitu wanavyoogopa na kuhofia sana, na wanahitaji kukombolewa kwavyo.

64 Katika siku ambazo Yeye alikuwa hapa duniani, moja ya sababu ambazo hawangeweza kumpokea Yesu wa Nazareti, na kumwamini Yeye na—na kupata ukombozi wao, kwa sababu ilikuwa isiyo ya kawaida sana kwao. Ilikuwa hivyo. Alileta ukombozi Wake. Mungu alikuwa amewatumia ukombozi. Nao ulikuwa usio wa kawaida sana kwao, hata ha—hawakutaka kuukubali, kwa sababu haukuja jinsi tu walivyozoea kuipokea dini.

65 Na ni hali nzuri sana iliyoko vile vile leo hii, ni la kuvutia sana kuona mlinganisho wake. Watu wa siku hizi wanashagaa, "Yuko wapi Mungu aliyeifungua Bahari ya Shamu? Yuko wapi Mungu aliyewaponya wenye ukoma? Yuko wapi Mungu aliyewafanya mateka wakimbie. . .huru?" Na hata hivyo liko papa hapa, nao hawataki kulipokea. Kwa nini? Sababu ile ile waliyokuwa nayo. Ni kinyume sana. Si ya kawaida. Wao, wao wanataka. . .

66 Katika siku hiyo, kama angeliwaletea kanuni za imani ama utaratibu fulani waliopaswa kupitia, taratibu fulani za dini na kadhalika, wangelipokea kwa furaha. Lakini kwa sababu alilileta jinsi ambavyo alilileta, watu hawakutaka kulipokea kwa njia ambayo alilileta.

67 Ndivyo ilivyo leo hii, vivyo hivyo hasa. Wao, wanaitaka, lakini hawataki kulipokea kwa kiwango ambacho Mungu hulileta. Nayo hiyo ndiyo njia ya pekee aliyo nayo Mungu ya kulileta. Wala hatuwezi kumshusha Mungu kwenye kiwango chetu cha mawazo. Inatubidi kukifikia kiwango

Chake cha mawazo, na kukutana Naye kwenye misingi ambayo ametuwekea ya kukutana Naye. Mnaona? Wanataka ukombozi.

68 Walikuwa na kanuni zao zote za imani za kimadhehebu, na Mafarisayo, na Masadukayo, na Waherodia, na kadhalika, namna zote mbalimbali na makundi ya dini potovu. Na kila mmoja, mmoja alikuwa na lake; kwamba hakuamini katika ufufuo wowote, wala Malaika wala roho. Huyo mwingine aliamini katika yote mawili, ufufuo, Malaika na roho. Na mmoja aliamini katika njia fulani ya kunawa mikono yako, na jinsi ya kufanya.

69 Kama tu ilivyo siku hizi. Sasa kama tungeweza kuinuka, Kristo angekuja katika aina fulani ya kitu kama hicho, vema, watu wangefurahi kukipokea.

70 Lakini ajapo katika Nguvu Zake za kufufuka Kwake, kuwafanya watu waishi na kutenda na kujiadabisha, na ku—kubadili mitazamo yao, kubadilisha njia zao, kubadilisha maisha yao, hawataki uhusiano wowote nalo.

71 Wanataka kuishi kama tu vile wanavyotaka kuishi. Na wanataka kuendelea kuishi jinsi ambavyo wameishi sikuzote, lakini hata hivyo wawe wa kidini sana, na waende kanisani na kuwa wafuasi wake, hata wanaweza kwenda Jumapili asubuhi au wakati wowote ule; na kuwa na mahubiri ya dakika kumi na tano kutoka kwa mchungaji; ambayo itawaendesha kutoka hapo, wameridhika nusu kwamba wamefanya dini yao kwa ajili ya juma hilo. Hilo latosha, warudi na kufanya chochote watakacho, juma zima.

72 Sasa, Mungu aliahidi katika siku hizi kile ambacho angefanya. Nami ningependa kumwuliza mtu yeyote, mhudumu yeyote, mahali popote, juu ya ahadi moja ambayo Mungu alilifanyia Kanisa, na kile Yeye alisema wangefanya, ila kile Kanisa halisi linafanya sasa. Lakini hawakitaki. Hawakitaki.

73 Yesu alimleta Mungu kwa maisha ya wanadamu. Mungu alifanyika mwanadamu. Wakati Yesu alipozaliwa, Mungu alifanyika mwanadamu, ili aweze kushirikiana na mwanadamu na katika mwanadamu, kufikia (nini?) kutimiza kusudi moja, ambalo ni, kumletea mwanadamu kile Mungu alicho; sio kile kanisa lilicho, lakini kile Mungu alicho. Yesu alikuja apate kumwasilisha Mungu kwa mwanadamu. Wala mwanadamu hakutaka.

74 Roho Mtakatifu huja siku hizi, vivyo hivyo, kuwasilisha Mungu kwa mwanadamu; lakini mwanadamu anataka kwenda kanisani. I—i—inanyamazisha mawazo ya—ya—yake. Hawezi—hawezi kuelewa Hilo. Nasi hatuna budi kujua kwamba Mungu hajulikani kwa dhana za kiakili. Mungu anajulikana kwa Kuzaliwa upya, na Roho Mtakatifu, si kwa njia nyingine yoyote. Yesu, Biblia imenukuu wazi kwamba, “Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo, isipokuwa kwa Roho Mtakatifu.” Na ikiwa

hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu, hujui kwamba Yeye ndiye Kristo, kwa kuwa hiyo ndiyo njia pekee anayojifunulia.

75 Huongoki mpaka umpokee Roho Mtakatifu. Biblia ilisema hivyo. Baada ya Petro kuokolewa na kutakaswa pia, akapewa Nguvu za kutoa pepo wachafu, na kuhubiri Injili; Yesu alimwambia waziwazi kwamba hakuwa ameongoka, mpaka alipompokea Roho Mtakatifu. Akasema, "Utakapoongoka, basi waimarishe ndugu zako." Huo ulikuwa ni ule usiku wa usaliti, kwamba alikuwa bado hajaongoka. Wala hakuna mtu aliyeongoka kweli mpaka amebadilishwa, na akafa kwa nafsi yake, naye Roho Mtakatifu ana mamlaka juu ya mtu huyo. Hawataki kufanya hivyo.

76 Sasa Roho Mtakatifu hatajikosesha adabu kwa mtu mmoja, na kujiadabisha kwa mwingine. Atamfanya kila mtu aingie katika tabia Yake, mnaona, kwa sababu ni Roho anayekuongoza. Analeta, anakufanya uwe chini ya asili Yake. Humtiishi chini ya asili yako; Yeye hukutiisha chini ya asili Yake. Naye Roho Mtakatifu anakufanya uishi na upende kuishi. Loo, jinsi unavyopenda kuachana na mambo ya ulimwengu, Roho Mtakatifu anapoingia! Jinsi anavyokutakasa na kukuosha, na kuweka shauku ndani yako ku—ku—kumfuata, na kiu na njaa ya kuwa na Yeye kwa zaidi, unajiosha tu. Yeye analeta uhalisia.

77 Sasa, wakati Mungu alipomweka mwanadamu hapa, na katika siku za Bwana Yesu, Yeye—Yeye alimpa mwanadamu ramani ya kweli ya kuzifikia Nguvu Zake.

78 Ramani ya barabara ni kitu kinachokuambia, kinachokuambia njia unayoelekea, ukitaka kwenda. Tutakapoondoka katika siku chache zijazo. . .Nimevuka nchi hii sana, mimi na mke wangu tulishangaa sana kuliwazia. Kwa miaka michache iliyopita, ungeweza kutaja ni wapi unataka kwenda, naweza kukuambia barabara yoyote inayoelekea huko, na katika muda wa dakika kumi na tano utawasili, kutoka hapa hadi California. Sijakosea hata wakati mmoja, katika sijui. . . Wakati mwingine kikamilifu kabisa, mnaona, kuhesabu muda wangu wa kuendesha gari, na muda wastani. Nimekuwa tu huku na huku, na juu chini, na kwenda na kurudi, mpaka unajua tu.

79 Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka tulijue Neno Lake. Tunalijua! Tumelipitia. Tumelijaribu. Tumelijaribu, na unajua linakoelekeza. Sasa ramani Yake ya barabara ni Biblia Yake. Biblia ndiyo ramani ya barabarani inayoongoza kwenye Nguvu za Mungu; imani inakuongoza kwenye zile Nguvu. Nguvu hutoa ahadi. Tunahitaji Nguvu.

80 Sasa, siku chache zilizopita, wakati mimi na Dada Wood, na mke wangu, tulipokuwa tumeketi chumbani, tukizungumza juu ya Ubatizo. Kuna wengi sana wa ndugu zetu wa thamani hapa, ambao tunamshukuru Mungu kwamba amewapa Roho Mtakatifu, kama vile Ndugu Willard Collins huko nyuma, pia—

pia nadhani Ndugu Hickerson, na—na wake zao, na Ndugu Charlie Cox na mkewe, na—na Ndugu Mike Egan nyuma hapa, na, loo, ni wangapi zaidi, ambao wamempokea Roho Mtakatifu. Na imeanza kuwa jambo la kuzungumziwa miongoni mwetu. Loo, Huyo na atuhuishe kufikia mahali ambapo tutaenda kutafuta, tukiona njaa na kuvuta tupate kweli za Mungu. Mungu ni kweli.

81 Sasa, ramani ya barabarani inatuelekeza wapi? Walipaswa kujua. Yesu alisema, katika zile siku alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Enyi wanafiki!" Alisema, "Mnaweza kutambua anga vizuri wakati mnaposema zimetanda na ni nyekundu, kwamba kesho kutakuwa na dhoruba; na kama kuna kianga, mnaweza kuitambua anga; lakini ishara za wakati, hamwezi kuzitambua. Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua na siku Yangu."

82 Hivi Biblia haikusema kwamba haya mambo yatatokea wakati Yeye atakapokuja? Je, nabii Isaya hakuyatabiri? Je, Yeremia, Ezekieli, manabii wote wadogo, hawakuyazungumzia? Kila kitu, ramani hiyo ya barabara ikielekeza moja kwa moja kwenye kikomo kimoja! Na wakati Yeye alipokuja, walikuwa wameyajaza makanisa yao kanuni za imani na kadhalika mpaka wakashindwa kuona ukweli wa kile alichokijia; kumleta Mungu ndani ya mwanadamu, kumfanya Mungu katika mwanadamu, kuwaunganisha pamoja tena.

83 Hata Ayubu, katika siku za dhiki yake, alipaza sauti, "Loo, laiti ningalimwona tu Yeye!" Kwa maneno mengine, "Laiti ningeweza kwenda nyumbani Kwake na kuubisha mlango Wake! Laiti ningeweza kupata mtu ambaye angeweza kusimama katika pengo kwa ajili yangu!" Kasema, "Najua sijatenda dhambi. Lakini hata hivyo, najua mimi ni mwenye haki, najua kwamba sijafanya chochote, kwa maana nimesimama juu ya sadaka ya kuteketezwa." Lakini alikosa uhalisi. Alikuwa na mfano, ila alikosa uhalisi. Akasema, "Loo, laiti ningepata tu Mtu ambaye angeweza kuweka mikono Yake juu ya mtu mwenye dhambi na Mungu mtakatifu, na kumletea kweli!" Wakati, yeye akiwa ni nabii na katika Roho, akiketi, akiyakwaruza majipu yake, Roho wa Bwana alikuja juu yake, radi zikamulika, ngurumo zikanguruma, naye akapaza sauti, "Najua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi; ingawa mabuu ya ngozi yameuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu!" Haya basi, kweli! "Atakuja siku moja." Kwa nini . . . Wale wazee wetu, na huko nyuma, ambao walitazamia hilo!

84 Naye Yesu akasema, "Mngalinijua Mimi, mngeliijua siku Yangu." Yeye alikuja kumuunganisha Mungu na mwanadamu pamoja. Yeye alikuja, huyo Mmoja tu. Malaika hangeweza kufanya hivyo. Hakuna mtu angeweza kulifanya isipokuwa Yeye. Yeye alikuja kufanya Mungu na mwanadamu, mmoja.

85 Alisema, "Siku hiyo mtajua kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Yeye alikuja kumleta Mungu na mwanadamu pamoja. Ambapo, mwanadamu alifanywa msaidizi wa Mungu, naye mwenyewe akawa ni mungu wa dunia. Hiyo ni kweli. Lakini alipoteza asili yake, kupitia kwa dhambi, nayo damu ya mafahali na mbuzi haingeweza kufanya upatanisho kwa dhambi hii. Lakini Damu ya Yesu Kristo ingeweza kufanya hivyo! Loo, vipi . . .

86 Unaona, Yeye, Yeye huonyesha ramani ya barabara. Yeye, Yeye alithibitisha Hilo. Ramani ya barabara iliongoza moja kwa moja kwake. "Kama mngalimjua Musa, mngelinijua Mimi pia. Kama mngelijua Neno!"

87 Wakati Shetani alipokutana Naye, Shetani alijaribu kumzungusha. Alichukua ramani ya barabara, Shetani alichukua, akaitoa, akasema, "Unaona, hapa inasema *hivi* hapa."

Akasema, "Lakini pia imeandikwa . . . "

88 Loo, kuna njia nyingi za kupitia, hii, *ile*, ama ile *nyingine,* "Loo, mradi tu ninafanya *hivi*." Hilo silo! Wewe, unapaswa kumpata Mungu katika uhusiano wa kibinafsi na ujuzi. Kama ukidai unayo, na bado unaishi kwa ajili ya ulimwengu, basi kuna kasoro. Ibilisi amekuzungusha kwa Maandiko yasiyo sahihi.

89 Tukiifuata ramani ya barabara, kama inasema "geuka kwenye barabara kuu fulani hapa," geuka hivyo! Kama Matendo 2:38 ilisema, "Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi," Halikugeuka kushoto; kwamba inakubidi kugeuka hivyo. Sijali jinsi ilivyo, inakubidi kuifuata barabara. Ikiwa Yeye alisema, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu," hiyo haikumaanisha ni kwa wakati uliopita. "Wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie," ndivyo lilivyosema! Hiyo ni ramani ya Mungu ya barabara. Lazima tuifuate. Barabara imewekwa alama.

Unasema, "Nitajuaje kwamba niko juu yake?"

90 Nyayo za miguu zilizolowa Damu za Bwana Yesu zilitengeneza hiyo barabara, nao wanafunzi walikaa kwenye msingi uo huo. Naye Roho Mtakatifu akawaelekeza. Fuata ramani hiyo ya barabara.

91 Basi siku chache zilizopita usiku, mtu fulani alisema, "Chini ya upambanuzi, Ndugu Branham yuko sawa. Lakini linapofikia suala la theolojia yake, yeye yuko nje kabisa." Mtu yeyote ambaye angejua tu kwamba Biblia inafundisha neno lenyewe *nabii* linamaanisha "mtabiri wa Neno." Ishara hizo ni ba—bakshishi tu. Walimu, na kadhalika, wanaweza kufundisha Neno. Lakini unapoona kitu fulani kikija ambacho ni cha kimbinguni na kinatabiri jinsi hiyo, inathibitisha tu kwamba kitu ndicho hicho. Hilo ni Neno la Mungu.

92 Yesu wa Nazareti, wakati alipokuwa hapa duniani, watu walimfuata mara nyingi kwa ajili ya samaki na mikate, na kadhalika, na kile wangeweza kupata kutoka Kwake. Akawaacha waendelee. Umaarufu Wake ukaanza kuongezeka mara moja. Ndipo siku moja akawakusanya watu akiisha kuwalisha watu elfu tano, akaenda ng'ambo ya ziwa. Kundi moja lilikusanyika nyuma Yake, likiambatana Naye. Naye akasema, "Kwa nini mmekuja? Sio kwa sababu ya muujiza, lakini kwa sababu ya samaki na mikate, ndiyo sababu mmekuja." Loo, wengine wao walidhani watakosa kitu fulani, mnajua, kama—kama hawakwenda kuona kile alichofanya. Lakini kukigusa? Hapana, bwana.

93 Ndipo Yesu, katika mlango uo huo wa 6 wa Yohana Mtakatifu, akaanza kuweka Injili chini, nao wakamkasirikia. Na tangu wakati huo, umaarufu Wake ukaanza kupungua, kushuka, "Hakuwa Yule yule wakati ule."

94 Na kama tu mhubiri wa kisasa au mtu fulani, ikiwa wangesema, "Mbona, ngoja kidogo hapa, una—unawaudhi watu kwa mahubiri Yako. Wewe, hupaswi kufanya hivyo." Sasa mhubiri wa kisasa angesema, "Loo, naam, afadhali niangalie kile ka—ka—kanuni ya imani inasema." Mnaona? "Labda ni afadhali nitazame nione kile kanisa linasema juu ya Hilo, kwa sababu huenda wakanifukuza."

95 Huyo hakuwa ni Bwana wetu. Bwana wetu alikuja kufanya mapenzi ya Mungu pekee! Alilifuata Neno. Na mtu yeyote aliye na Mungu ndani yake ataifuata njia ile ile. Je, aliacha? Hapana, bwana. Hata hivyo, umaarufu Wake—Wake ukazidi kupungua wakati wote. Wengi hawakutembea na Yeye tena. Walimwacha. Mlango unaofuata, wengine zaidi waligeuka. Ndipo mlango unaofuata, wengine zaidi wakageuka. Alikuwa wapi? Akienda Zake Kalvari! Lakini aliwahi kusimama? La, bwana. Kamwe hakupatana kwa Neno la Mungu, hata kidogo. Aliongoza moja kwa moja kwenye barabara kuu. Aliifuata ramani ya barabara. Yeye, kulikuwa na barabara iliyowekwa mbele Yake, na barabara hiyo hana budi kuikanyaga.

96 Kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ana barabara iliyowekwa mbele yako. Inakubidi kuifuata barabara hiyo. Mungu anaiweka alama. Imewekwa alama kwa Damu. Naye Roho sikuzote huishi katika Damu, kwa sababu kupitia Damu huja Uhai; seli ya Damu ndiyo seli ya Uzima. Sasa tunamfuata basi, na tunaona jinsi ramani ya barabara inavyotuongoza, inaonyesha tunaelekea njia gani. Daima imekuwa hivyo. Ni njia ya Mungu iliyotolewa kwa ajili yetu. Neno ni njia ya Mungu iliyotolewa.

97 Mtu anapofikia mahali ambapo anayaona Maandiko, na kwa sababu ya kupendwa na watu, kwa sababu ya ushirikiano wa kanisa fulani, kwa sababu watu wake

hawatamruhusu kulihubiri, mtu huyo kamwe hataendelea na Mungu. Inakubidi kurudi na kulichukua Neno hilo, haidhuru ni nini. Usipolichukua, u—uko kando kwenye mzunguko mahali fulani, utazama katika matope ya udongo ya dhambi. Ninampa changamoto mtu yeyote.

98 Na kwenye maktaba yangu huko juu, tuna historia zote za kale nijuazo, *Wazee Waliotangulia Nikea,* ya—ya—yale *Maandishi ya Kale* ya Josephus, *Babeli Mbili* kilichoandikwa na Hislop, *Kitabu Cha Foxe Cha Wafia Imani,* maandishi mengi, mengi sana ya kale. Wala hapajawahi kuwapo na wakati ambapo kanisa lilijifikisha mahali ambapo lilisimama kwenye kanuni zake za imani, ambapo Mungu aliliinua tena. Lilizama pale pale katika matope ya udongo. Hiyo ni kweli. Kamwe halikuendelea, kiroho, kamwe halikuendelea wala halitaendelea kamwe. Si mpango wa Mungu.

99 Mpango wa Mungu ni Roho Mtakatifu. Ndio njia iliyowekwa na Mungu ya kufanya mambo. Sasa angalieni hili. Katika siku za Nuhu. . .mpango wa Mungu sikuzote ni njia ya mateso. Hiyo ndiyo sababu watu hawautaki.

100 Katika siku za Nuhu, walikuwa na dini. Walishakuwa nayo kwa miaka elfu mbili, kama vile tumekuwa na Ukristo. Na kulikuwako na wakosoaji kama kulivyo nao sasa. Na katika siku za Nuhu, ilikuwaje? Tunaona ya kwamba Nuhu alisimama mlangoni mwa safina, naye akajenga safina ambayo ilikuwa ni kinyume cha mawazo yoyote ya binadamu. Kamwe mvua haikuwa imenyesha, kamwe hakukuwa kumewahi kuwako na wingu angani. Lakini Mungu akasema itanyesha. Hilo lilikuwa ni Neno la Mungu. Mungu alisema, “Ijenge safina.” Naye Nuhu akajenga safina, na kusimama kwenye mlango huo mmoja na kuhubiri wokovu. Na hiyo ndiyo tiba pekee kwa ajili ya wokovu.

101 Ni mfano wa jinsi gani leo hii! Kunao mlango mmoja unaoelekeza kwa Mungu, na huo mlango ni Kristo. Kristo ni Roho Mtakatifu anayeishi ndani yetu. Nasi tunasimama mlangoni pa safina ya Mungu, ya Roho Mtakatifu, na kuhubiri “Hii ndiyo njia,” ramani ile ile ambayo hao wengine walipitia.

102 Nuhu alikuwa njia ya Mungu iliyoandaliwa. Katika siku za ukombozi kutoka Misri, Musa alikuwa ndiye njia ya Mungu, mnaona, huduma ya kimbinguni, nji—njia. Mnaona, Nuhu alikuwa na kitu kilichokuwa tofauti. Nuhu alikuwa na dini iliyokuwa tofauti na hizo zingine; alikuwa na Neno la Mungu. Nao watu hawakuzoea Neno la Mungu. Walikuwa na kanuni zao za imani, walikuwa na yale waliyotaka. Kwa hiyo ilikuwa—ilikuwa ni kanuni za imani walizokuwa wakisikiliza, wala sio Neno. Lakini Nuhu alikuwa na Neno.

103 Musa alikuwa na Neno. Haidhuru hao wengine walikuwa na nini, Musa alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Angalia kile kilicholithibitisha. Yeye alifanya ishara na maajabu, na kila

ishara na mwujiza ulikuwa na sauti. Sasa Mungu alisema, “Wasipoisikia sauti ya ishara ya kwanza, wataisikia sauti ya ishara ya pili.”

104 Sasa watu siku hizi, kama walivyokuwa katika siku za Yesu, wanafuata miujiza. “Loo, huenda Yeye akafanya kitu ambacho ni tofauti kidogo. Nisingeona hilo likifanywa. Hebu tuone kama Yeye anaweza kutambua *hiki*. Hebu tuone kama anaweza kulifanya.” Mnaona, hivyo ndivyo Yeye afanyavyo. Walifuata kwa sababu tu ya samaki na mikate. Lakini inapofikia kutubu, kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, na kumpokea Roho Mtakatifu, wasingeligusa Hilo. Hiyo ni kweli. Kisha wanakuhukumu.

105 Nao walimhukumu Yesu, kwa kusema, kasema, “Loo, unahubiri kinyume na haya.” Hilo halikumkomesha. Yeye aliendelea moja kwa moja.

106 Mhudumu mashuhuri, hivi majuzi, aliniwekea mikono, kasema, “Nitakuombea, Ndugu Branham, ya kwamba kamwe hutasema chochote dhidi ya vile watu hawa wanavyoishi katika makanisa haya.” Akasema, “Ndugu Branham, utawafanya... Utawafanya wote wakukasirikie.”

107 Nikasema, “Ninawezaje kujizuia, wakati Roho yangu ya ndani kabisa na nafsi yangu inalia dhidi yake?”

Akasema, “Vema, mimi sisemi lolote dhidi yake.”

108 Nikasema, “Huwezi. Una miradi ya mamilioni ya dola. Huna budi kupata dola zao. Hainibidi kuwa nazo.”

109 Kitu pekee ninachohitaji ni Nguvu za ufunuo wa Bwana Mungu. Huyo tu ndiye tunayemhitaji, Roho. Kusimama juu ya ile Kweli! Sijali ni madhehebu mangapi yanayolipinga, lingali ni Neno la Mungu. “Mbingu na nchi zitapita; Maneno Yangu hayatapita kamwe. Yeyote atakayeondoa au kuongeza lolote kwenye Kitabu hiki, huyo ataondolewa katika Kitabu cha Uzima, sehemu yake.” Ninaliamini jinsi tu ramani inavyosema. Hakuna lingine, njia ya Mungu!

Musa alikuwa na zile ishara. Alithibitisha kwamba alikuwa ni mtumishi wa Mungu.

110 Mungu sikuzote hupenda kutenda kazi kupitia kwa mwanadamu. Ni mpango wa Mungu kutenda kazi kupitia mwanadamu. Mnaamini hilo? Mungu hufanya kazi kupitia mwanadamu. Alimfanya mwanadamu msaidizi Wake duniani. Alimfanya mwanadamu mungu mdogo kuliko Yeye Mwenyewe.

111 Sasa tumepitia hayo katika mafundisho hivi majuzi, ya Mwanzo 1:26, ambapo Yeye alikuwa El, Elah, Elohimu, ajitoshelezaye kwa yote, anayeishi peke Yake. Halafu ndani Yake mlikuwamo na sifa za Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; sio miungu watatu, ofisi tatu ndani Yake kwamba Yeye ataishi kwenye vipindi hivyo vya wakati. Yeye alikuwa ni Mwokozi, alikuwa

ni Mfalme, alikuwa ni Mungu. Vitu hivi vyote vilijidhihirisha vyenyewe. Ni sifa za Mungu, mnaona, lakini, katika hilo, katika Yeye hapo mwanzo.

112 Basi hapo Mungu alipomwumba mtu katika sura Yake Mwenyewe, Yeye alimweka duniani kama mungu mdogo. Yesu alitangaza hilo hapo aliposema, "Si imeandikwa katika torati zenu, ya kwamba ninyi ni miungu?

"Na kama waliwaita hao miungu ambao Neno la Mungu liliwajilia," ambao walikuwa ni manabii, "mnawezaje kunihukumu Mimi wakati ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?" Yeye akasema. Mnaona? Kamwe wasingeweza kulielewa, mnaona. Lakini mwanadamu aliwekwa hapa akiwa na mamlaka juu ya dunia. Alikuwa na kila kitu chini ya mamlaka yake.

113 Kile Adamu alichopoteza, Yesu alithibitisha kwamba alikuwa amerudisha. Alikomesha maumbile. Aliwafufua wafu. Yeye, Yeye alifanya kila kitu. "Nao ulimwengu unaugua siku hizi," Biblia ilisema, "kwa ajili ya madhihirisho ya wana wa Mungu," kwa ajili ya Mungu kuingia katika watoto Wake tena katika uhalisi, kufanya mambo yawe halisi. Nalo linawakwaza watu.

114 Kama Shetani hawezi kuwazuilia Ukweli, yeye huwafanya mashupavu wa dini; anawatupilia mbali upande *huu* na upande *ule*, nao wanapata upuuzi wa kila namna, damu na mafuta, na mihemko, ambayo hata si ya Kimaandiko.

115 Lakini kaeni kwenye ramani! Kaeni kwenye barabara kuu. Kaeni kwenye Maandiko. Msiyaache. Hiyo ndiyo sababu Yesu alikuja, ili mwanadamu asidanganyike na kwenda kando ya njia, bali akae moja kwa moja ndani ya Neno. Yule Mtakatifu Paulo mashuhuri alisema, "Kama malaika akishuka kutoka Mbinguni na kuhubiri injili nyingine yoyote ila hii ambayo mumehubiriwa, na awe aliyelaaniwa kwenu." Naam, bwana.

116 Mbona, Shetani alishuka katika bustani ya Edeni kama malaika wa Nuru, na kumwambia Hawa. Mbona, kamwe ha—hakukana, yeye alisema, "Loo, vema, hilo ni sawa. Loo, hakika, Mungu amesema hilo; lakini, wajua, utakuwa na Nuru zaidi." Tuna nuru nyingi sana za Hawa siku hizi, na nuru za Shetani, kuona vitu. Nayo Biblia ilisema, "Katika siku za mwisho, ibilisi angejifanya mwenyewe malaika wa Nuru." Kanuni hizi zote za imani na madhehebu, na upuuzi huu wote unaoendelea. Ambao, nusu yake hata haina Maandiko yoyote kwake, angalau. Hiyo ni kweli.

117 Kaa kwenye barabara kuu. Kaa kwenye ramani ya barabara. Pitia njia waliyopitia wale wanafunzi, nenda kwenye Neno walilohubiri. Liishi! Lishuhudie, "Ninajua kwamba ni Kweli!" Ishara katika siku za mwisho, Mungu akiishi katika mwanadamu. Ni mpango wa Mungu.

118 Mungu hana budi kumpata mtu anayeweza kumtumainia, mtu ambaye Yeye anaweza—Yeye anaweza kuwa na imani naye; na—naye anaweza kuwa na imani na Mungu, ambaye anaweza kumwamini Yeye. Mnaamini hilo, sivyo? Hakika. Mungu hana budi, kupata mtu ambaye Yeye anaweza kumtumainia. Ndipo anapopata mtu kama huyo anayeweza kuweka matumaini Yake na Nguvu Zake ndani yake, mtu ambaye ataifuata barabara, ambaye atakaa moja kwa moja kwenye ramani, mnaona, asonge mbele mpaka afikie mahali pa Nguvu. Imani itamwongoza mahali hapo, kwa sababu yeye ana imani katika Neno. Itamwongoza kwenye ile ahadi, nayo ahadi... Itamwongoza kwenye Nguvu, nazo Nguvu zitamwongoza kwenye ile ahadi. Halafu basi wakati anapoipata ile ahadi na anaanza kudhihirisha, inafanya nini? Inayapofusha macho ya ndugu vuguvugu asiyeamini, anayezitumikia kanuni za imani. Hiyo ni kweli kabisa.

119 Hivyo ndivyo ilivyofanya kule, kule nyuma katika siku za Yesu. Yeye alisema, "Kama nisingalikuja, msingaliijua dhambi. Lakini sasa kwa vile nipo hapa..." Amina! "Sasa kwa kuwa nipo hapa, hamna udhuru."

120 Na, leo hii, kama Mungu alifanya ahadi Yake ya kwamba Yeye angemtuma Roho Mtakatifu katika siku za mwisho, na mambo haya yatukie, mngelitilia shaka. lakini sasa kwa vile Yeye amekuja na analitenda, ulimwengu hauna udhuru. Limenguruma kupitia taifa baada ya taifa, baada ya mahali baada ya mahali, hata likaifunika dunia. Hiyo ni kweli. Hawana udhuru. Wasingalilijua kama Mungu asingalikuja na kulileta. Lakini ametuletea sisi sasa, halafu basi katika uhalisi, uhalisi wa kulifuata Neno. Kuifuata ile Kweli! Dumu pamoja Nayo!

121 "Loo, ninaenda huku kwenye kanisa la Kibaptisti," wanasema, "tunayo ile Kweli." Methodisti wanasema, "Tunayo ile Kweli." Sasa ni ipi? Nyote wawili ni tofauti, ni lipi lililo na Kweli. Unashuka kwenye wa Adventista wa Sabato, "Tunayo ile Kweli." Unaenda kwenye Church of Christ, "Tunayo ile Kweli."

122 Vema, kuna njia moja tu kufanya ile Kweli, hiyo ni, dumu pamoja na hilo Neno. Mtu fulani aliliacha Neno mahali fulani. Wana sehemu ya Kweli, halafu wanaenda na kuweka mchepuko ndani Yake. Wanaingia kwenye barabara kuu, kisha wanachepuka. Dumu pamoja na Neno!

123 Wazungumzie juu ya ubatizo katika Jina la Yesu Kristo. "Loo, haileti tofauti yoyote."

124 Kweli inaleta tofauti! Paulo alisema aliwaamuru watu kubatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo. Alisema, "Kama Malaika akisema lolote lingine, na alaaniwe." Kweli inaleta tofauti!

125 Vipi kama Musa alisema, "Nitavua tu ninii yangu... Nitavua tu kofia yangu badala ya kuvua viatu vyangu. Ni vigumu

kuvifungua viatu vyangu, nitavua tu kofia yangu na kuonyesha heshima"? Mungu alisema, "Viatu!" Naye Mungu alihitaji viatu, si kofia; viatu, kile alichosema.

126 Mungu huamuru kila Neno Lake litimizwe kikamilifu. Halina budi. Inakupasa kufanya yale Yeye asemayo ufanye, kwa kuwa hakuna nukta moja wala yodi moja itakayopita kutoka Kwake. "Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatashindwa." Halina budi kukaa. Moja, yodi ama nukta haitapita kutoka kwa Hilo, Hilo lote halina budi kutimia.

127 Na, sasa, mwanadamu alikuwa ni raia wa Mungu. Mwanadamu ndiye Mungu anayemtumia kutenda kazi.

128 Ndipo mtu anapoipokea ile Kweli, anaingia kwenye barabara kuu ya kweli na kuanza kutembea, na kupata kweli hizi, zikisonga mbele, inafanya nini? Ndugu asiyeamini, yeye atamwangalia, ni kana kwamba yeye ni. . . Yeye, hawezi kulikubali. Akilikubali, hana budi kuliacha kanisa lake. Kama akiliacha kanisa lake, yeye anasimama peke yake.

129 Mhudumu fulani aliniambia, mara baada ya yale mahojiano kule juu, mhudumu alisema, "Angalia hapa!"

130 Niliwaambia jukwaani, nikasema, "Basi endapo nimekosea sana, kuna mamia ya wahudumu hapa, mtu fulani na aje anifundishe yaliyo kweli." Hamkumwona mtu akija, sivyo? Wala hamtamwona, kwa kuwa hayuko.

131 Mhudumu mmoja, mhudumu mashuhuri sana, nisingelitaja jina lake. Ni ndugu wa thamani. Yeye alikuja, kasema, "Ndugu Branham, huduma yako, hakika, unaweza kuendelea na kufanya hivyo. Lakini kama tukiyakubali Hayo, tukiyakubali Hayo, kanisa letu linatukataa, basi tutaenda wapi?"

132 Nikasema, "Kwenye Mahali pa kujificha patoshelezapo kwa yote, Kristo Yesu! Huko ndiko mtakakoenda. Nendeni kwa Kristo."

"Vema," akasema, "lakini huduma yetu?"

133 Nikasema, "Huduma yenu ni sawa tu na huduma ya mtu mwingine yeyote, ikiwa ni ya Kristo, haidhuru itawabidi kwenda wapi."

134 Kasema, "Vema, kama nikibatiza hivyo, wangenifukuza kanisani mwangu."

Nikasema, "Walinifukuza mimi. Kwa hiyo basi inaleta tofauti gani?"

135 Kaa tu kwenye barabara kuu. Fuata tu ile ramani. Bila shaka, endelea tu Nayo, haidhuru wana kitu gani.

136 Sauli alikuwa na jeshi lililokuwa limefunzwa. Sauli alikuwa na jeshi kubwa la kielimu. Wao, hawakumtaka Samweli; kama nilivyohubiri hapa wakati fulani uliopita, mahali fulani. Walikuwa na hilo jeshi kuu. Loo, hakika! Sa-. . . Naye Samweli

akawaambia, aliwapandisha kabla hawajamchagua huyu mfalme. Mungu alikuwa ndiye Mfalme wao.

137 Naye Mungu ndiye Mfalme wetu! Mbona tunataka kitu kingine chochote mbali na Mungu? Kwa nini Mkristo atake kitu kingine chochote kumwongoza ila Roho Mtakatifu? Sijui. Siwezi kuelewa.

138 Ndipo Samweli akawaita. Akasema, "Nataka kuwaambieni jambo fulani." Kasema, "Nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana, ila lile lililotimia?"

"La."

139 "Niliwahi kuchukua pesa zenu zozote? Niliwahi kuwaomba pesa?"

140 "La, hujatuomba pesa hata. Na yale uliyosema, Bwana aliyatimiza. Tunajua hilo."

141 Akasema, "Basi ni kwa nini mnamkataa Mungu, na kutaka mfalme? Mnataka kutenda kama ulimwengu."

142 Na hivyo ndivyo Pentekoste inavyofanya siku hizi. Inataka kutengeneza majitu ya kielimu. Inataka kuondoa Nguvu Kanisani. Inataka kufanya dhehebu likue, kuwaleta wafuasi wengi zaidi. Huo ni upuuzi! Basi unapomfunga mtu kwa kanuni ya imani, unapofanya hivyo, unamwondoa Roho Mtakatifu kutoka kwake. Itambidi kutoa mahali fulani. Roho Mtakatifu ataendelea mbele; huyo mtu hawezi, kwa sababu, ya kanuni yake ya imani. Sasa yeye alisema . . .

143 Halafu basi, hakika, Sauli alilifundisha jeshi lake. Loo, jamani. Aliwafanya hao Waisraeli kujua tu kila mbinu ya kuangusha mkuki, ama kufanya lolote. Lakini siku moja palitokea mpinzani, maskini Goliathi. Na, ndugu, ilihitaji zaidi ya mafunzo ya kielimu wakati huo.

144 Ilihitaji mtu aliyejua jambo fulani kuhusu ya kimbinguni. Lakini Mungu alikuwa na mtu kama huyo. Bwana ashukuriwe kwa jambo hilo. Mungu sikuzote anaye mtu fulani. Daima anaye. Alikuwa na mtu angaliweza kuweka mkono Wake juu yake. Maskini jamaa mwekundu huko nje, hakuwa wa maana sana, bali alipanda kule na kusema, "Kwani mnataka kuniambia ya kwamba mtamwacha Mfilisti huyu asiyetahiriwa kulichafua jeshi?" Na hapo alikuwapo mzee Sauli, tangu begani hata kichwani mrefu kuliko hao wote. Mafunzo yake yote ya kielimu hayakufaa kitu.

145 Sasa makanisa yamefanya jambo hilo. Wamemwacha Roho Mtakatifu. Wameziondokea Nguvu za Mungu. Wameondoka kwenye uongozi wa Roho. Nasi tuna ninii . . . Tunao wana wa—wa Kishi, pia. Ndio kwanza tuwe na mmoja wa majitu yetu makuu hivi majuzi, huku Afrika, alipewa changamoto na Mwislamu, kwenye Maandiko. Ilikuwaje? Yeye alichukua maji

kama yule mwana mwingine wa Kishi; sio kumdharau ndugu yetu.

146 Lakini walikuwa na mtu aliyejua ya kwamba Mungu angeweza kukomboa. Wakamleta maskini Daudi mdogo kule juu, naye akasema, “Sijui lolote juu ya mikuki yenu, mafunzo yenu ya kielimu. Ila najua jambo moja. Ninajua jambo moja, nilimfuatilia kondoo aliyechukuliwa na adui. Uh-huh, Uh-huh. Mungu akaniwezesha kuwarejesha.” Akasema, “Ni zaidi sana vipi Yeye atanifanya, atanijalia, kumrudisha Mfilisti huyu asiyetahiriwa!”

147 Tunachohitaji siku hizi ni wanaume na wanawake wanaotaka uhalisi. Haleluya! Sio kanuni ya imani; uhalisi, huo ndio ulimwengu unaohitaji leo hii! Sio kanuni za imani na mitindo; tunahitaji uhalisi katika Mungu! Walimwengu hawautaki. Walimwengu hawautaki. Hawataki, hawataki kuukubali. Lakini Kanisa halina budi kuwa Nao. Mungu anawatakeni mwe Nao. Yeye ni Mungu wa uhalisi. Naam, bwana.

148 Hivi majuzi usiku, nilienda pamoja na marafiki fulani ambao wako sasa, kundi lao, huku nje kuiona hii, hii hapa *Samsoni na Delila*, sinema ya Cecil B. DeMille. Nilisikia mengi sana kuihusu. Nikawazia nitaendesha huko nje, nione ilivyofanana. Nilipoiona hiyo, nilianza kushangaa kile Mungu alichoona katika jamaa kama Samsoni, katika siku za waamuzi.

149 Mnaona, Mungu humtumia mwanadamu. Mnaamini hilo? Lakini Yeye anaweza tu . . . Anaweza tu kumtumia mtu wakati anapoweza kumpata mtu, anapoweza kumpata mtu ambaye anaweza kumtumia. Kulikuwako na kipindi katika siku za waamuzi, Yeye asingeweza kumpata mtu. Jambo pekee angaliweza kufanya, lilikuwa ni kusimama tu, kisha angepitia njia fulani; kisha kumwinua mwingine, naye angepitia njia fulani. Hakuwa na mtu ambaye angeweza kuweka matumaini halisi ndani yake.

150 Nami nikashangaa, Yeye aliona nini katika Samsoni huyu? Samsoni alikuwa kama wengi wa viongozi wetu siku hizi, mwanamume wa wanawake, akiwaandama mahali mahali, akiwafuatilia wanawake. Kama wengi wa viongozi wetu siku hizi, kama wengi wa wanaopatana kwenye Neno, wanamwachilia mwanamke awaongoze, wanawaingiza ndani wawe wahubiri na vitu kama hivyo. Loo, jamani!

151 Ninamwuliza tu mtu yeyote kutoa Maandiko kwa ajili ya mhubiri mwanamke. Ninaweza kuwathibitishia ya kwamba katika Agano la Kale, kama alivyosema Paulo, “Ndivyo isemavyo Torati.” Nilikuwa nikiangalia kwenye kumbukumbu la Agano la Kale, jana, nami nikakuta mle ndani ambamo walikuwa na polisi maalum, kwamba mwanamke hata asingeweza kuja kwenye ua wa pili wala wa tatu, sembuse

mimbarani. Walikuwa na polisi maalum Hekaluni, kuwaweka Mataifa huko nje, na baadaye wanawake, kisha wakaja Walawi, halafu kwenye Patakatifu pa patakatifu. Hata wasingeweza kuja kwenye ua wa pili. Hiyo ni kweli kabisa. Na siku hizi tumewafanya wanawake sanamu zetu. Wengi mno wa viongozi wetu wanawaacha wanawake warembo na kadhalika namna hiyo kuwashawishi, acha urembo wa—wa mwanamke wa kiroho, kanisa.

152 Mnajua, mwanamke ni mfano wa Kanisa. Sisi ni Bibi-arusi. Kanisa ni Bibi-arusi.

153 Kuna bibi-arusi wengi sana. Nao wanawaacha hao wanawake wawashawishi. Wahudumu siku hizi wanayaacha hayo makanisa yawavute kuwatoa kwenye ile Kweli. Naye anafanya nini? Anakata nywele zake, anakatilia mbali nguvu za mwanamume, mwanamke anafanya apendavyo.

154 Siwapingi dada zangu. Kama Mungu angalimpa mwanamume kitu bora kuliko mke, Yeye angalimpa hicho.

155 Lakini sio wanawake wote ni wake, sio wanawake wote. Sio wanawake wote ni mama. Sio wote walio na watoto ni mama. Nimeona wengine ambao walikuwa na heshima bora zaidi kwa mbwa; wanawachukua watoto wao na kuwaweka mtaani, na kulala mle. Watu wakitoka nje wamevaa maskini nguo hizi fupi na kadhalika, wamevalia kizinifu.

156 Niliwaona wanaume wakishuka mtaani, jana. Nilikuwa nikienda sehemu ya chini ya mji kununua kitu fulani, huko nikaona mwanamume baada ya mwanamume, akishuka mtaani, na maskini mke wake mrembo, amevaa maskini nguo fupi sana, walionekana wa kuchukiza sana. Huyo si mwanamume; huyo ni dondoadume. Mtu yeyote atakayemwacha mke wake kuvaa namna hiyo, huyo si mwanamume sana. Loo, huenda akawa na misuli, kitu kama hicho; huyo ni hayawani, huyo ni mnyama.

157 *Mwanamume* ni "tabia." Yesu, Mwanamume mkuu kuliko wote aliyepata kuishi, Yeye alikuwa ni jamaa mdogo tu, "hana uzuri hata tumtamani," lakini kamwe hapajakuwapo na tabia iliyowasilishwa duniani kama ya Yesu Kristo.

158 Nimeona wanaume fulani, wenye uzito wa pauni mia mbili na hamsini, hawakuwa na wakia hata mmoja wa mwanamume ndani yao. Inapofikia . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kamwe asiwe na nguvu kama farasi. Wakati mwingine hawana akili ya farasi, kwa hiyo, akili ya farasi ya mambo. Farasi angejua vizuri zaidi. Sasa, hiyo ni kweli. Sasa, hebu jaribu tu kumwacha farasi dume ajaribu kumvamia jike, uone kinachotukia. Farasi ana akili bora zaidi. Mnaona? Wala mwanamume hana akili kama farasi alivyo nayo inapofikia maisha mengi.

159 Nasi tunamwita maskini nguruwe kizee, tunamwita nguruwe jike, na maskini mbwa wa kike, mchafu. Na wengi wa hawa wanawake wenye uso mrembo huku ni duni zaidi,

machoni pa Mungu, mara milioni kumi, kuliko maskini mbwa mchafu ama nguruwe. Hiyo ni kweli kabisa!

160 Hilo linasikika lisilopendeza, hiyo ndiyo sababu watu hawalipendi. Hapo ndipo Yesu alipowaambia Ukweli, wakamwacha. Lakini majira yamewadia, na sasa yapo, ambapo Baba anataka kitu cha kumwabudu Yeye katika Roho, na kutembea katika Roho, na kuishi katika Roho, na kusema Kweli.

161 Kweli sikuzote, ama inakuweka huru, au inakufunga. Kama umefungwa, basi wewe si huru. Iwapo wewe ni huru, hutakuwa ukiishi jinsi hiyo.

162 Unasema, "Vema, ninaye Roho Mtakatifu," na ungali unaishi vile vile unavyoishi? Jambo fulani limekupata. Kamwe hukumpata Roho Mtakatifu aliyekuja kwenye Siku ya Pentekoste; alikufanya tofauti.

163 "Siamini katika kunena kwa lugha. Siamini katika uponyaji wa Kiungu. Siamini katika mambo haya." Basi kamwe hukumpata Roho Mtakatifu aliyeshuka kwenye Pentekoste. Hakika hukumpata!

164 Ulibatizwaje? "Nimebatizwa!" Vipi, katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu? Si ajabu unatenda jinsi unavyotenda! Unaona?

165 Paulo akasema, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

166 Wakasema, "Tayari tumeamini. Sisi ni Wabaptisti." Matendo 19, angalieni kama hiyo si kweli. "Sisi ni Wabaptisti! Tumebatizwa na Yohana," a—akasema, "mtu yule yule aliyembatiza Yesu."

167 Akasema, "Huo hautafanya kazi." Kasema, "Inawapasa kuja na kubatizwa tena, kama kamwe mnataka kupata Roho Mtakatifu." Huenda ukapata kitu kinachoonekana kama Yeye, kitu kinachotenda kama Yeye, kidogo; bali si Kitu halisi, maana, inakupasa kuja na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Basi walipofanya hivyo, yeye aliweka mikono yake juu yao, ndipo *basi* Roho Mtakatifu akaja juu yao. Walidhani walikuwa Naye.

168 Nami ninataka kujua, huyo ndugu hapa aliye kanisani, ama mahali ilipokuwa, alisema ya kwamba Kiyunani asilia hakisemi; "mnampokea Roho Mtakatifu *wakati* mnapoamini," alisema Kiyunani kilisema hivyo. Ninataka ujue kwamba hilo ni kosa. Hilo ni kosa; si hata Kiyunani, si Kiebrania, wala hata si Kiaramu. Kilisema, "Mumempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?" Sio, *wakati* mlipoamini. Kwa hiyo yeyote aliyekwambia hilo, hujui kile unachozungumzia, ndugu. Mnaona? La, bwana. Unampokea Roho Mtakatifu "baada" ya kuamini, sio *wakati* unapoamini.

169 Roho Mtakatifu ni karama ya Mungu, inayokuja juu yako, inayokubadilisha na kukufanya kwa jumla tofauti na vile ulimwengu ulivyo na jinsi watu wengine walivyo. Wewe ni fotauti! Wao. . .Haikubidi kuvalia tofauti hata kidogo, haikubidi uvae ukosi uliopinduliwa na joho refu. Unaishi tofauti. Unatenda tofauti. Nguvu za Mungu ziko pamoja nawe. Watu wanajua, umetiwa alama popote uendapo. Vema. Mungu anawajua walio Wake. Yeye huwatia alama walio Wake. Jambo ndilo hilo. Bali huna budi kuja kwenye ile Kweli. Unaona.

170 Ni kitu gani kilichokuwa ndani ya yule Samsoni? Mwandama wanawake? Hakika. Alikuwa mwenye kiburi, asiyetii baba na mama yake. Walimwambia asishuke kwenda kule pamoja na mwanamke huyo, huyo Yezebeli, bali asingewasikiliza. Ilikuwa ni kitu gani? Samsoni alikuwa na nguvu. Sasa sikilizeni. Samsoni alikuwa yuko tayari kuzitoa nguvu zake. Samsoni alimpa Mungu nguvu zake, bali akampa Delila moyo wake.

171 Basi hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Sasa, wanaume wengi wataenda kwenye seminari na kusoma, loo, jitu la kielimu, wajifunze Kiyunani chote na kadhalika; lakini, inapofikia kwenye ile Kweli, yeye atampa Bwana nguvu za elimu yake, naam, ila moyo wake analipa kanisa, na si Mungu. Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, wanataka kufuata kanuni zao za imani.

172 Hawataki uhalisi wa Roho Mtakatifu. Hawataki kutenda tofauti hata kidogo na vile watendavyo sikuzote. Lakini unapokuwa Mkristo, wewe ni mtu wa kipekee, ukuhani wa kifalme, taifa la kigeni, watu wa kipekee, unafanya mambo ya kipekee na mambo ya kigeni, yasiyofaa kwa ulimwengu. Na wakati ukiwa katika ulimwengu, wewe hufai kwa Mungu. Mmoja ni kinyume na mwingine. Mmoja anakufanya utende kama watendavyo Mbinguni, huyo mwingine anafanya kama watendavyo duniani.

173 Nao watu wanataka kufanya kama watendavyo duniani, kisha wanaendelea na kusema wanaenda Mbinguni, lakini ni kuvunjwa moyo jinsi gani hayo yatakavyokuwa. Yesu alisema, "Wengi watakuja Kwangu, kwenye siku hiyo. Watasimama kwa makumi ya mamilioni, na kusema, 'Nimekuwa mfuasi wa *hili*, na nimefanya *hili*.'" Yeye akasema "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Mnazitumikia kanuni za imani."

174 Laiti ungaliongozwa na Roho! Wana wote na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu. Wanaenda kwa Roho, wa kipekee, wa kigeni. Wanakaa sawa, na kila tendo liko pamoja na Biblia. Wanadumu, mafundisho yao yote yanadumu moja kwa moja na Biblia. Hawatatofautiana kwa jambo moja. Ambapo Biblia inalisema, watasonga waingie ndani yake moja kwa moja. Kama wakisimama kwa dakika moja, wanajaribu kuchunguza waone wataendea njia gani; ndipo Roho Mtakatifu analifunua, naye anasonga mbele moja kwa moja. Naye anafanya jambo lile

lile, anafuata masharti yale yale, anaweka msingi ule ule, Mungu yeye yule anakuja juu yake, na maajabu yale yale, na miujiza ile ile, na ishara zile zile zinamfuata, zilizomfuata Yeye.

175 Yeye alisema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, nikiwa Mwanadamu, aminini kazi nifanyazo. Niaminini Mimi. Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Mnaona, kuna kazi zinazoambatana na imani hii. "Nionyeshe matendo yako (kwa ninii yako) pasipo imani yako, nami nitakuonyesha matendo yangu kwa imani yangu," alisema Paulo. Mnaona?

176 Sasa, ni kitu gani kilichokuwa ndani ya Samsoni? Asingesalimisha moyo wake.

177 Leo hii, wanadamu wanawazia zaidi juu ya kanuni zao za imani kuliko vile wao . . . na watu wanawazia zaidi juu ya kanuni zao za imani. Vema, sasa, sisemi chochote dhidi ya makanisa.

178 Ninazungumza juu ya pentekoste! Ambayo, kanisa hili linaegemea kwenye pentekoste. Si dhehebu la Kipentekoste. Sisi si wafuasi wa dhehebu lolote, kamwe hatukusudii kuwa. Sisi ni mali ya Kristo. Hiyo ni kweli. Halafu, sasa, Pentekoste si dhehebu. Pentekoste ni ujuzi ambao watu hupokea. Methodisti waliupokea. Katoliki iliupokea. Wabaptisti wanaupokea. Mtu yeyote anaweza kuupokea, bali ni ujuzi.

179 Na kuna maelfu na maelfu, wanaojiita, "pentekoste," hata hawajui ujumbe wa kwanza wa pentekoste ni upi. Kabla hujapata kuanza vizuri, huna budi kuja juu ya msingi sahihi. Huna budi kusimama kwenye msingi wa kipentekoste. Msingi wa kipentekoste ni nini?

180 Wakati kule kuzinduliwa kwa Kanisa kulipotolewa kwenye Siku ya Pentekoste, wakati walipowaona wakinena kwa lugha, naye bikira Mariamu akiwa huko akitenda kana kwamba alikuwa mlevi, na hao wengine wote wakiyumbayumba huko namna hiyo, wao walisema, "Nini? Kitu gani, hiki? Hawa wote wamelewa?"

181 Petro akasema, "Hawa hawajalewa, kama mnavyodhania, kwa kuwa ni saa tatu ya mchana. Hili ni lile lililonenwa katika . . . kwenye ile ramani, huko nyuma kwenye ramani ya barabara. Hili ni lile ambalo ramani ya barabara ilisema. Yoeli alisema tutapafikia mahali hapa, tutafika kwenye hii njia panda, 'Itakuwa katika siku za mwisho, siku mbili za mwisho, miaka elfu mbili ya mwisho, asema Mungu, Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu na binti zenu watatabiri, na juu ya wajakazi wangu na watumishi wa kike, vijana wenu wataona maono, wazee wenu wataota ndoto. Nitaonyesha maajabu na ishara katika mbingu juu, na vitu kama hivyo.'"

Wakasema, "Tufanye nini tupate Hili?"

182 Utaweka msingi wa aina gani, Petro? Unazo funguo za Mbinguni. Yeye akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtampokea Roho Mtakatifu yule yule. Ahadi hii ni kwa kila kizazi kitakachofuata baadaye, kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Huo hapo msingi.

183 Mnaona, wao—wao watakuja na kutoa ninii za—zao. . . Wataenda kwenye. . .Wataenda shuleni. Wavulana wataenda shuleni, kujifunza kuwa mhudumu. Ambalo ni sawa, sina chochote dhidi ya hilo, kujifunza kuwa mhudumu; lakini, huwezi kujifunza kuwa mhudumu, karama ya mhudumu ni karama itokayo kwa Mungu. Hao mitume walikuwa werevu na wenye elimu sana waliyoweza kuwa nayo, Yesu bado. . .Yeye. . . Hawakuwa. Lakini bado asingewaruhusu kuhubiri mpaka walipompokea Roho Mtakatifu. Ndipo wakati walipompokea Roho Mtakatifu. . .Sasa, ukienda kwenye seminari, na ujuzi waliopata kwenye Pentekoste unakuja juu yako, amina. Lakini kama ukitokea tu kupitia dhana za kielimu na, loo, bingwa wa Kiyunani na mtaalamu wa sanaa, na vitu hivi vyote mbalimbali, Sha—Shahada ya Kwanza, na mambo haya mengine yote. Kama ukitoka na digrii hizo, unatoa tu nguvu zako za elimu yako. Unataka kuutoa moyo wako kwa Mungu. Mungu anautaka moyo wako. Naam, bwana. Alitoa nguvu zake, si moyo wake. Naam, bwana.

Mungu anaweza kutumia tu kile tunachompa.

184 Sasa wapo wengi wenu watakaosema, “Nitatoa dakika kumi na tano Jumapili asubuhi kama ninii. . .Kama ukihubiri muda mrefu kuliko hapo, nitaninii tu, itanibidi kusimama na kwenda nyumbani.” Vema, una dakika kumi na tano Jumapili asubuhi. Hummf! Hizo ndizo unazompa Mungu. Baadhi yao walisema, “Labda ninaweza kuvumilia nusu saa. Sijui vile ninavyoweza kufanya hivyo.” Vema, mnaona, hizo ndizo unazopata, dakika kumi na tano, nusu saa. Mnaona?

185 Unaweza kutoa nini? Mungu atapokea utakachompa, bali Mungu anakutaka wewe wote. Anataka kila sehemu yako. Anataka yote. Anataka kila kitu ulicho wewe. Anataka maisha yako. Anataka ushuhuda wako. Anataka kila dakika unayoishi. Anakutaka uishi sawa, utende sawa, uongee sawa, utende sawa. Anataka kila kitu kisalimishwe kikamilifu Kwake, ili aweze kukuongoza na kukuelekeza, na kukuweka mahali ambako anakutaka uende. Kuongozwa na Roho!

186 Lakini watu siku hizi husema, “Sasa ngoja kidogo, kama mchungaji wangu akihubiri zaidi ya dakika ishirini!”

187 Nimesikia hilo mara nyingi. Nimeona wachungaji wazuri wakifukuzwa makanisani, kwa sababu halmashauri ya mashemasi ilisema, “Sasa angalia hapa, kasisi, tulikuajiri

uje hapa. Wala hatukukuajiri kuja hapa na kutukemea asubuhi nzima. Tunawatakeni, tu—tumeweka wakati wa dakika ishirini; kengele inalia, na afadhali uwe umemaliza!"

188 Mnajua, ni—ni—ningependa kuwa na kanisa kama hilo wakati mmoja. Ningependa kuwa na majaliwa ya kuwaambia kile ninachowazia juu yao na kile Neno lisemacho kuwahusu. Naam. Mbona, kama ilichukua siku nzima, endelea tu kuhubiri. Naam. Mungu anataka kujitolea kukamilifu. Mnaamini hilo? Mungu anataka kujitolea. Mungu anawezaje kukuonyesha uhalisi kabla hujajisalimisha Kwake? Huna budi kujisalimisha. Sikilizeni.

189 Unaposalimisha yote! Unaimba huo wimbo, "Natoa yote, natoa yote." Vipi kuhusu hizo sigara? Na hayo mavazi je? Na hasira hiyo je? Na mambo hayo mengine yanayoambatana nayo? Vipi kuhusu tabia hiyo ndogo uliyo nayo? Vipi kuhusu maskini wazo hilo la udaku? Vipi kuhusu huko kumkemea mtu yeyote anayebatiza katika Jina la Yesu?

190 Wakati, huna mahali popote katika Biblia ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa kwa njia nyingine yoyote. Nampa changamoto mtu yeyote kunionyesha ambapo mtu yeyote, wakati wowote nje ya kanisa Katoliki ambapo walianza miaka mia tatu baada ya mtume wa mwisho, ambapo mtu yeyote alipata kutumia jina "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" katika ubatizo. Njoo unionyeshe hayo Maandiko ama hiyo historia. Ni kanuni ya imani ya Katoliki! Si ya Kiprotestanti. Sasa, ninaweza kuwaonyesha katika Biblia ambapo Biblia inatabiri ya kwamba wangetumia Jina Lake mpaka wakati huo, nao wakatokea na jina la uongo kwamba "wako hai," na—nao wamekufa. Ninaweza kuwaonyesha hayo kwa Maandiko. Biblia ilisema kwamba wangefanya hivyo.

191 Hapa limeletwa moja kwa moja machoni pao, kwa nini watu wasilichukue? Kama tu vile walivyofanya hasa katika siku za Yesu. Hawataki uhalisi. Wanataka kanuni ya imani. Wanataka kitu, cha kutumia, waseme, "Mimi ni mfuasi wa mahali *hapa*. Mimi ni wa kusanyiko *hili*. Ni mfuasi!" Ati nini?

192 Unataka kuwa wa Mbinguni! Huko ndiko shauku zako zinakopaswa kuwa, katika mambo ya juu. Yesu alisema, "Yatafakarini mambo yaliyo juu, sio mambo yaliyo katika nchi. Yatashindwa." Dumu pamoja na Mungu. Dumu na uhalisi. Mungu ni Mungu wa uhalisi. Sikuzote amekuwa hivyo, katika nyakati zote. Wakati wowote ambapo mwanadamu alipata kutembea na Mungu, Mungu alifanyika uhalisi ambao ulifanya ishara na maajabu na miujiza pamoja na watu Wake. Ni kusudi la Mungu kufanya hivyo. Kusalimisha yote.

193 Papa hapa Louisville, Kentucky, sio muda mrefu uliopita, kulikuwako na familia nzuri sana ya watu. Walikuwa na

mtoto mchanga mgonjwa. Wakapiga simu akaombewe. Daktari akatoka hospitalini. “Basi vipi kuhusu mtoto huyu mchanga?”

194 Akasema, “Mtoto huyo yuafa. Hakuna kitu kingine anachoweza kufanyiwa.” Kasema, “Ana lukemia.” Kasema, “Huyo mtoto hana budi kufa.”

195 Akawazia, “Ee Mungu, hujasema hilo bado. Kamwe hukushuhudia hilo.” Nikaenda nikazungumza na hao wazazi, nao wazazi walikuwa wakilia na kuomboleza. Mtoto wa—wa—wao alikuwa ameondoka, kadiri walivyojua. Lakini walifanya nini?

196 Huyo daktari alikuwa sahihi. Yeye, kila kitu alichojua jinsi ya kufanya, alikuwa amekifanya. Lukemia ni mwuaji, na hakuna kitu kinachoweza kuukomesha. Kasema, “Huyo mtoto atakufa.”

197 Maskini huyo babu wa mtoto huyo. Nyote mnakijua kisa hicho. Basi maskini babu wa mtoto huyo akaja. Aliponisikia nikizungumza kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, yeye alisema, “Nilikuwa nikikumbuka miaka mingi iliyopita, wakati maskini mhubiri mmoja aliposema kungekuja wakati ambao watu wangempokea Roho Mtakatifu tena, na ishara na maajabu yangetokea.” Akaingia kwenye chumba kidogo peke yake. Asingekaa pamoja na mwanawe wala mkwe wake tena. Alikaa mle ndani, akilia na kuomba. Wakati jamaa huyo mzee alipotoka huko, jasho likining’inia kwenye paji la uso wake wenye upara, macho yake yakimetameta. Akasema, “Mtoto huyo ataishi.”

Kasema, “Ati nini?”

198 Akasema, “Daktari, nakuheshimu kama—kama mtu wa sayansi. Ninakuheshimu na elimu yako ambayo umesomea kupitia utafiti wa tiba. Lakini,” kasema, “niliomba na kuomba, na nikaomba mpaka nikasalimisha kila kitu kilichonibidi kusalimisha, ndipo Roho Mtakatifu akasema, ‘Mtoto huyo ataishi.’” Aliishi. Kwa nini? Alisalimisha kila kitu alichokuwa nacho.

199 Mungu alimshika na angeweza kuongea naye, wakati alipokuwa radhi kusalimisha kila kitu. Hicho ndicho tumepungukiwa. Hutaki kuzisalimisha njia zako. Hutaki kusalimisha mashirika yako. Hutaki kusalimisha maskini kikundi hicho kidogo ulichomo. Hutaki kusalimisha wakati wowote, inakubidi kufanya *hiki, kile,* ama *kinginecho,* badala ya kuomba. Hutaki kusalimisha vitu kwa Mungu. Mungu anakutaka usalimishe! Tukifunga, nataka kusema hivi. Mambo mengi sana hapa ningetaka kusema, bali sina wakati. Mungu anataka kujisalimisha kikamilifu. Unaposalimisha kila kitu, basi utajua kile ninachozungumzia ni Kweli.

200 Nawe unasema, “Wangenifukuza kanisani mwangu. Wasingeniruhusu kuhubiri.” Hilo linaleta tofauti gani? Hilo ni shirika la kisayansi. Kile tunachozungumzia, ni kutembea katika Roho. Mungu ni wa hakika.

201 Vipi kama Musa angalisema, “Sasa ngojea. Nimeelimika katika mbinu zote za hili, wachawi, na kadhalika, huko Misri. Ninaweza kuwafundisha hao Wamisri mbinu cha—cha—chache. Ninaweza kuwafundisha saikolojia. Ninaweza kuwafundisha maadili ya—ya mambo mengi. Mimi ni bingwa wake”? Lakini ilimbidi kusahau kila kitu alichowahi kujua. Naye Mungu akararua tu kila kitu kutoka kwake; ilimchukua miaka arobaini kufanya hivyo. Lakini wakati alipokutana na Mungu, uso kwa uso, alijua kulikuwako na Mungu aliye hai. Alimwona katika kichaka kilichowaka moto, na akaongea Naye. Yeye alishuka na kufanya kazi yake yeye mwenyewe, haikumbidi kuwa na jeshi. Alishuka, yeye pamoja na Mungu. Aliifuata ramani ya barabara. Alikuwa na nguvu za Mungu. Alikuwa na ahadi ya Mungu. Alikuwa na Roho wa Mungu. Hakuhitaji maadili wala elimu yake.

202 Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, ilimbidi kutafuta, tena, kumpata mtu. Alienda kwa watu wa tabaka la juu, wenye elimu na wenye akili, je, angeweza kupata mtu yeyote? La, bwana. Walimwita, “Beelizebuli, ibilisi.” Asingeweza kupata mmoja ambaye angelimfuata. Alifanya nini? Ilimbidi achukue walio bora sana angaliweza kuwapata. Hiyo si ni huzuni?

203 Mara nyingi nimewazia jambo hili. Nasi tunafunga, enyi kanisa, sikilizeni matamshi haya. Sikuzote nimewazia ni kitu gani, kitu gani, mbona, jinsi tumejinyima, jinsi tumemwibia Mungu mpango Wake, kwa, kutoyasalimisha maisha yetu kikamilifu Kwake, kila tulicho nacho, Kwake. Jinsi ambavyo ha—hatujakubaliana na mpango Wa—Wake. Jinsi ambavyo tumekawia, na tumemfanya Yeye kungojea na kungojea, na kungojea, akijaribu kumpata mtu fulani ambaye angeweza kumtumia kufanya kazi, akijaribu kumpata mtu mahali fulani ambaye Yeye angemtumaini, mtu fulani ambaye angesalimisha kila kitu.

204 Aje kwa njia ya akili timamu, ya busara kwa Mungu, aseme, “Baba, mimi hapa. Sijali, nitayafuata Maandiko, ile ramani. Sijali yale mtu mwingine yeyote asemayo, nitadumu Nayo,” na alimaanishe kweli. “Sijali itanigharimu nini, Bwana. Mimi si kitu, kwanza, bali ninataka Wewe uniongoze. Pia jalia Roho Mtakatifu, aliyeiandika Biblia hii, na kufanya ahadi hizi, alithibitishe kupitia maisha yangu. Ninajisikia ya kwamba Wewe unaniongoza kwa njia hiyo.”

205 “Mimi hapa, nitume mimi,” alisema Isaya hekaluni, wakati alipowaona Makerubi wenye mabawa juu ya nyuso zao, juu ya miguu yao, na wakiruka kwa mabawa. Naye akatwaa kaa la moto na kukisafisha kinywa chake, ndipo Roho wa Mungu akaja juu yake. Mbona tusiweze? Mungu hawezi kumpata mtu kama huyo.

206 Wakati alipowatafuta wanafunzi Wake, “Alikuja kwa walio

Wake Mwenyewe, walio Wake hawakumpokea." Asingeweza kumpata mtu yeyote. Walikuwa wakingojea Hilo.

207 Leo hii ulimwengu unangojea uponyaji wa Kiungu. Lakini sijali ni kiasi gani cha uponyaji wa Kiungu m—mnaofanya, wangali hawatawaamini.

208 Vema, mara baada ya kumkataa Yesu, wakati wale sabini walipoondoka, hata aliwageukia hao wanafunzi, kasema, "Mnataka kwenda, pia?"

209 Wao wakasema, "Twende wapi?" Petro, yeye alisema, "Wewe unayo Maneno ya Uzima wa Milele." Mnaona?

210 Naye akatoka moja kwa moja, na kulikuwako na mtu ambaye hata hakuwa na mboni za macho kwenye matundu yake. Ndipo akatengeneza udongo na kuyapaka macho yake, akamwambia, "Nenda kaoshe kwenye birika la Siloamu." Basi, alipofanya hivyo, alirudi akiona.

211 Hilo liliwabadilisha? Umaarufu wake uliongezeka? La. Ulishuka chini, chini, chini. Kwa nini? Yeye alikaa kwenye barabara. Alikaa kwenye ramani ya barabara.

212 Ndivyo ilivyo siku hizi. Wanaona ishara, maajabu, miujiza, na kila kitu kikitendwa, nao wanasema, "Ah, hilo, hakuna kitu kwa hilo. Lingalitendeka, kwa vyovyote vile." Mnaona?

213 Walimfufua Lazaro kaburini, ilionekana kana kwamba hilo lingalilitikisa taifa zima. Biblia ilisema Yeye angefanya hivyo. Hizo zilikuwa ni ishara zilizokuwa zifuate. Wakati Yeye aliposimama, kwa yule mwanamke Msamaria hapa, na kusema, "Unao waume watano." Hilo lilipaswa kuutikisa ulimwengu wote.

214 Naye anasimama leo hii katika watu Wake, nanyi mnamwona, wakati baada ya wakati, akifanya jambo lile lile. Nao wanasema, "Aa! Uh-huh. Vema, nadhani hilo lilikuwa ni vema." Mnaona, kwa urahisi tu hawahusiki, hakuna kujisalimisha. Loo, wanachangia muda mfupi, wanaenda kanisani mara chache tu, na kitu kama hicho. Lakini inapofikia kujisalimisha, la, hawatafanya hivyo, hawatajisalimisha. Hawataki.

215 Wakati Yesu alipowaita wanafunzi Wake, ilimbidi kufanya nini? Akawachukua wale wasio na elimu kabisa, wanaume, watu ambao hata wasingeweza kuandika jina lao wenyewe. "Petro, Yohana," Biblia ilisema, "Walikuwa wasio na elimu wala maarifa." Hao ndio ilimlazimu kuwachukua.

216 Lakini kama wenye akili wasingetaka, wasingemsikia wakati huo, hawatamsikia sasa. Wana njia zao wenyewe. Wako kwenye barabara yao wenyewe. Na wao—wanaifuata barabara hiyo kwa sababu wamefunzwa hivyo, kwa sababu wachungaji wao, maaskofu wa—wao, na makadinali wao na—na mapapa, na wowote wale, waliwaelekeza kwenye barabara hiyo.

217 Lakini Roho Mtakatifu atakurejesha kwenye Pentekoste, kila wakati. Walifanya hivyo katika Maandiko, kwa kila mtu, na itakuwa hivyo katika siku hii, kwa kila mtu. Atakurejesha kwenye uhalisi huo. Atakurejesha kwenye ubatizo wa Nguvu za Roho, ambaye atakuongoza wala hataondoa Neno moja kutoka kwenye Biblia. Atadumu moja kwa moja katika Biblia. Mahali Hiyo inaposema *hili*, Yeye atalifuata moja kwa moja. Roho Mtakatifu atalifuata. Analeta uhalisi.

218 Yeye alifanya nini? Ilimbidi kuwachukua hawa wavuvi wasio na elimu, hata hawakuwa na nguo; kitu fulani tu walichojizungushia, aproni ya wavuvi, na kadhalika, hakuna nguo. Wasio na elimu kabisa, wasingeweza kuandika jina lao; hawakusoma, hawana elimu. Lakini Yeye alimpata mtu fulani. Ilimbidi kumchukua mtu. Lakini alikuta watu katika hali ya namna hiyo, waliokuwa tayari kujisalimisha, waliokuwa tayari. Hawakuwa na kitu kingine cha kushikilia. Hawakuwa na makanisa yoyote, madhehebu yoyote na chochote kile. Walikuwa ni wavuvi tu wasio na elimu, wachunga kondoo; hawakujua kuandika, hawakujua kusoma, wala chochote kile. Lakini hawakuwa na cha kupoteza, ndipo akawachukua nao wakajisalimisha kwake. Wakasema, "Lolote usemalo Wewe, Bwana, tutalifanya. Tutakufuata Wewe."

219 Lakini walipojisamisha kabisa na wakajitolea kwa Mungu, Mungu aliwapa uhalisi wa kipentekoste. Akawaongoza hadi Pentekoste, na kuwapa Roho Mtakatifu. Hapo, mahali walipokuwa, hapo, chini ya Roho wa Mungu, wakifanya kila namna ya ishara za kijinga kwa watu, wakigugumiza na kugugumiza, na kupiga makelele, na kujaribu kuninii . . . Biblia ilisema. Walikuwa juu ya nini? Walikuwa kwenye barabara kuu.

220 Biblia ilisema, "Kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha zingine nitasema na watu hawa, na hii ndiyo Raha, ya nafsi. Hiki ndicho kile kitu kitakachokuja." Isaya 28:18, isomeni. "Kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha zingine nitasema na watu hawa. Hii ndiyo Raha." Si Jumapili; si siku ya Raha. Roho Mtakatifu ndiye siku ya Raha. Ninyi ndugu wa Adventista; siyo sabato ya siku ya saba ndiyo Raha. Roho Mtakatifu ndiye Raha! "Kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha zingine nitasema na watu hawa. Na hii ndiyo Sabato. Hii ndiyo!" *Sabato* inamaanisha "Raha." Hii ndiyo Raha, kwa nafsi, unayo Raha ya Milele.

221 Kama vile Mungu, hapo alipoumba ulimwengu. Siku ya saba, Yeye alipumzika baada ya hapo. Alipumzika, akaendelea kupumzika.

222 Tunapoingia katika Mungu, tunapumzika wakati wote; si kutoka Jumapili moja hadi nyingine. Tunapumzika, Milele. Tunao Uzima wa Milele. Roho Mtakatifu hukupa Raha.

223 Sasa, walikuwa na ujuzi wa kipentekoste, uhalisi wa Mungu. Walikuwa wamepata kitu fulani.

224 Hebu niseme jambo moja zaidi. Kanuni za imani haziridhishi moyo ulio na njaa. Kanuni za imani hazitaridhisha. Kama mtu ana njaa kwa ajili ya Mungu, nawe umwambie, useme, “Kariri Kanuni ya Imani ya Mitume, jiunge na kanisa, andika jina lako *hapa,* nyunyiziwa ama uzamishwe,” ama chochote utakacho, hilo kamwe halitaridhisha nafsi iliyo na njaa. Maana, walikusudiwa tangu zamani, na Mungu, wapate kuutafuta Uzima. Wakati mmoja walikuwa ni malaika, wakati mmoja kulikuwako na malaika ambaye hakuanguka. Theluthi mbili za malaika wa Mbinguni walianguka; hao ni hawa pepo wachafu wanaotenda kazi miongoni mwa watu, ni wa kidini sana. Mnajua Biblia inasema hivyo. Nyinyi hamkuwa tu hapa nyote siku zote. Wakati mmoja mlikuwa mahali pengine.

225 Kumbukeni, dhambi haikuanza duniani. Dhambi ilianza Mbinguni, wakati Lusifa alipochukua na kujifanyia. . . Yeye alisema, “Nataka dhehebu, kufanya kitu kikubwa mno,” akaenda kwenye nchi ya kaskazini na kuanzisha kitu kikubwa kuliko alichokuwa nacho Mikaeli. Ndipo akatupwa nje kutoka Mbinguni.

226 Nao hao malaika huko nyuma, hao pepo. Vema, hiyo ndiyo sababu, “Maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tayari tunayo moja inayongoja.” Mnaona? Na hiyo ndiyo sababu, “Jina letu liliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu.”

227 Mnawezaje? “Mna macho, wala hamwezi kuona; masikio, wala hamwezi kusikia.” Si ajabu, mnaona. Hapo, mambo haya yote, mnaona, ambayo Mungu aliahidi huko nyuma, yote yalikuwa. . . Wakati niliposema hivi majuzi usiku ya kwamba mtu. . .

228 Yesu alisema. Mnyama aliyekuja juu ya nchi, yule mpinga Kristo, akiwa ni wa kidini sana, “zitafanana sana ingewadanganya walio wateule kama yamkini.” Lile kuu, jinsi lile dhehebu kuu lingeanza, nao wangekuwa na madhehebu mengine. Maskini yule mama kahaba; naye alikuwa na binti wadogo, waliokuwa ni makahaba waliotoka, madhehebu. Kasema, “Nao karibu wataudanganya ulimwengu mzima, na wadanganye hata walio wateule kama yamkini.”

229 Ila haiwezekani; majina yao yaliwekwa juu ya Mwana-Kondoo. “Wale aliotangulia kuwajua, Yeye amewaita; wale aliowaita, amewahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, amewatukuza.” Kwa hiyo, hakuna tena, mnaona. Hiyo ni kweli. Huwezi kuja Mungu asipokuita. “Si yeye atakaye wala yeye apigaye mbio; ni Mungu arehemuye.” Hiyo ni hakika. Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema ndivyo.

230 Halafu, hawataki kusikia Hilo. Kwa nini? Wako gizani. Wanataka kufuata kanuni ya imani. “Mimi ni mwema tu kama ulivyo wewe.” Hakuna kitu kilichosemwa kuhusu wema. Hakuna mtu aliye mwema. Mungu ndiye aliye mwema, mnaona. Lakini je, wewe uko tayari kujisalimisha Kwake? Hilo ndilo ninalofikiria. Uko tayari kujisalimisha? Unaona? Haita—haitaridhisha nafsi iliyo na njaa. Sikilizeni.

231 Wakati, Paulo, ni wangapi wanaojua ya kwamba alikuwa mwa—alikuwa mwanatheolojia? Lakini alikuwa bingwa wa kielimu. Yeye, hakika, yeye alifundishwa chini ya Gamalieli, mmoja wa wanatheolojia hodari sana wa siku hizo. Lakini alisema nini wakati alipokuja kwa Kanisa? Someni Wakorintho wa Pili 2:4, katika Wakorintho wa Pili 2:4, alisema, “Sikuja kwenu kwa maneno ya ufasaha, hekima ya mwanadamu wa ulimwengu huu; kwa maana, kama ningelifanya hivyo, matumaini yenu yangejengwa juu ya hekima ya mwanadamu, mashirika, madhehebu. Lakini nimekuja kwenu katika Nguvu za Roho Mtakatifu, madhihirisho. Madhihirisho ya nini? Akionyesha ishara na maajabu kwa Roho Mtakatifu. Nilikuja kwenu kusudi. . .kusudi ma—matumaini yenu, kusudi imani yenu, isiwe juu ya hekima ya dhehebu fulani kubwa la kanisa fulani, bali iwe juu ya Nguvu za Roho Mtakatifu na kufufuka kwa Yesu Kristo.” Mwanatheolojia mkuu sana aliyepata kuishi, alisema ilimbidi kusahau kila kitu alichopata kujua, kusudi ampate Kristo. Naye alisema, “Sihubiri mambo ya kielimu. Ninahubiri urahisi wa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Nami nilikuja kwenu, nikiuhubiri Huo.” Kasema, “Ningeweza kuhubiri kwa njia hiyo nyingine, lakini” kasema “kazi zangu na ka—kazi zangu si kuhubiri namna hiyo.”

232 “Sasa, tutaona ikiwa hatuwezi kupata milioni moja zaidi katika mwaka wa ’34, ’44,” chochote kile, misemo yao. “Tutakuwa na *idadi fulani* ya wafuasi watakaojiunga mwaka huu!”

233 Yeye alisema, “Ningeweza kufanya hivyo. Nilikuwa na hilo muda mrefu sana, lakini nikaliacha. Nilikuja kwenu, sio kwa maneno makuu ya kupendeza ya mwanatheolojia fulani. Lakini nilikuja kwenu katika Nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu, kusudi imani yenu ijengwe katika Roho Mtakatifu bali si katika hekima ya watu fulani.” Loo, jamani!

234 Mungu, anawatafuta watu kama hao. Mungu anatafuta leo hii watu ambao anaweza kuwashika namna hiyo.

235 Si muda mrefu uliopita, huko London, Uingereza; nikifanya matembezi kidogo. Nayo Uingereza ni, Visiwa vya Uingereza, vimejaa watu sana! Huko Uingereza, ni vigumu kupata mahali, ni vigumu, ila palipo na nyumba, nao wanawalea nanii wao. . . Kama vile katika Ujerumani, na kadhalika, hizo huko ni nchi za kale, nayo ardhi imepungua sana, nao wana shamba dogo. Huko

Ujerumani na mahali kama hapo, hupati, kwenye ua wa nyuma, nyasi nzuri iliyokatwa pamoja na miti mingi. Unapata nyanya na maharagwe na viazi, chakula. Hawana budi kufanya hivyo. Nayo ardhi imetumiwa sana mpaka . . .

236 Maskini askari Mwingereza aliyekuwa akinitembeza, tulipanda juu ya kilima, mimi na Ndugu Baxter, na mvulana huyu. Tukafika mahali palipokuwa ni pa kupendeza. Kulikuwako na miti, na nyasi chanikiwiti, na kila kitu. Nikawazia, "Hapo si ni mahali pazuri!" Ndipo nikamwambia huyu Mwingereza, nikasema, "Bwana, ni—ningetaka kukuuliza swali. Ninaona kwamba kisiwa chenu hapa kimefunikwa kabisa. Kwa nini mahali pakubwa hapa, penye ekari kadhaa, mahali pazuri penye miti na bonde, na kadhalika namna hiyo, kwa nini mpaache hapo, na hakuna mtu angaliweza kujenga nyumba hapa?"

237 Akasema, "Kasisi, na—nataka kusema jambo hili. Yapata miaka mia mbili iliyopita, kulikuwako na janga la homa ya maji meusi, iliyotokea hapa Uingereza." Kisha kasema, "Hawakuwa na chanjo, nao watu wakafa kama nzi." Akasema, "Mikokoteni, wananiambia, ilikuja usiku na mchana. Hata wasingeweza kuwazika. Makasisi wangekuja tu huku nje, mara moja moja, ainue mikono yake na kuomba, kisha anarudi. Waliwatupa wote kwenye bonde hili hapa. Wasingeweza hata kuwazika." Kasema, "Walikufa, na wakafa, mpaka maelfu mara maelfu, ya watoto, watu wazima, matineja na kila kitu, wakafa. Nao wakawapeleka tu huko nje, kisha wakawachukua tu na kuwanyunyizia udongo juu yao wakati hilo pigo lilipokuwa limekoma."

238 Kisha akasema, "Unajua nini?" Akasema, "Tangu siku hiyo, hata wa leo, Mwingereza ana hakika sana hataweka msingi wake ambapo kitu kama hicho kilipokuwa. Hataweka msingi wake juu vitu kama hivyo . . . Kamwe hataweka nyumba yake mahali ambapo mauti yalikaa namna hiyo." Ndipo nikasimama pale kidogo, nami nikawazia. Hakuna haja ya kumwambia, asingelielewa.

239 Lakini jinsi, ulimwenguni, kwamba mtu atakabili kwa uaminifu sana, hata, kama homa nyeusi, miaka mia mbili iliyopita, ilikuwa kwenye ardhi hiyo, lakini una shaka sana, na kujijali sana hata inakubidi kuishi kwa muda mrefu kidogo, na huenda ukaambukizwa homa nyeusi kama uliwahi kujenga nyumba yako pale, halafu utaweka kikomo chako cha Milele juu ya kanuni fulani za imani zilizobuniwa na mwanadamu aliyekufa mamia ya miaka iliyopita, juu ya theolojia fulani, theolojia ya kanisa fulani ambayo imekuwa kwenye rafu kwa mamia ya miaka, hakuna kitu, hakuna matendo ya Mungu ndani yake, na kila kitu kingine, nawe utabandika jina lako na kanuni ya imani, na kila kitu, moja kwa moja hapo, na kuendelea kuishi. Sikiliza, ewe rafiki, kamwe usifanye hivyo.

240 "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Tazama, niko pamoja nanyi, hata ndani yenu, sikuzote, hata ukamilifu wa dahari; Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele."

241 Mungu ni Mungu wa uhalisi. Kamwe usichukue tu kanuni ya imani. Usichukue tu mhemko. Chukua uhalisi! Mchukue Mungu halisi, kitu alicho Mungu, Mungu wa uhalisia. Hilo linakupa hakikisho. Linakupa matumaini. Linakupa imani. Linakupa Roho. Linakupa ishara. Linakupa maajabu. Linafanya ndani yako kama tu lilivyofanya ndani ya Kristo. Kwa sababu, hilo lilikuwa ndilo kusudi Lake la kuja, kumleta Mungu kwa mwanadamu, na likamfanya Mungu na mwanadamu mmoja.

242 Ila sisi tulichukua madhehebu, na tukamfukuza Yeye; tukachukua kanuni za imani, na kumfukuza, na sasa tuko kwenye barabara ya kando hapa. Lakini kuna barabara kuu ya kweli hasa, na "njia" katika hiyo barabara kuu.

243 Sasa kwenu ninyi ndugu Wanazarayo, ningetaka kusema jambo hili. Mnasema, "Barabara kuu ya kale iliyobarikiwa."

244 Lakini haikuwa ni barabara kuu, kama mkiangalia. Lilisema, "Kuna njia kuu, na," *na* ni kiunganishi, "na njia." Nayo "hiyo njia" iko kwenye hiyo barabara kuu. Si wote wako kwenye barabara kuu, wakienda, bali wote walio kwenye "njia," ndio wanaokwenda. Mnaona? "Ipo njia kuu, na . . . " Someni Isaya 35, "Kuna barabara kuu, na njia." Mnaona? Barabara kuu ina sehemu ya katikati, iko katikati ya barabara. Na katikati ya barabara ndipo. Ndipo mvua ijapo, huosha takataka zote pembeni.

245 Sasa kama mtaangalia, mtu anapoongoka, anaweka, macho yake moja kwa moja kwa Kristo. Sasa usipoangalia, kama nilivyokuwa nikihubiri hivi majuzi usiku, kama katika . . .

246 Wakati Yakobo na Esau walipozaliwa, wote wawili walizaliwa na baba mtakatifu na mama mtakatifu, lakini walikuwa ni mapacha. Mmoja, mtu wa kimwili, wa kidini, alienda kanisani na alikuwa ni mtu mzuri, mzuri sana. Yakobo alikuwa kidogo ni laghai, ila alilenga nia yake kwenye jambo moja. Haki hiyo ya mzaliwa wa kwanza ilimaanisha kila kitu kwake, haidhuru jinsi ilivyombidi kuipata. Kwa sababu, Biblia ilisema, "Yeye alichaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuiangalia hiyo."

247 Na siku hizi kuna watu, sijali itawabidi kutumia umaarufu kiasi gani, ni kiasi gani itawabidi kupoteza, ama yale inayowabidi kufanya, haileti tofauti yoyote kwao kama wanaitwa wa mtindo wa kale, haidhuru wao ni nini, wameyaelekeza macho yao kwa Kristo kwa sababu walichaguliwa kwa Uzima wa Milele. Nao wakapanda pale pale

juu ya hilo. Kama itachukua kila kitu, kama itachukua kila kitu walicho nacho, wanapanda pale.

248 Huyo mwingine ni mtu wa kawaida. Anaenda kanisani na kujisikia vizuri tu kama hao wengine, anaenda nyumbani. Mnaona, hayo ni maisha ya Esau, unaona. Nayo hayo mengine ni maisha ya Yakobo. Sasa haya basi, pande zote mbili.

249 Panda msingi wako katika Kristo Yesu! Hakikisha kwamba ni katika Yeye. Unaingiaje ndani Yake? Kwa kupeana mikono, kwa kunyunyizia, kwa kitu gani? “Kwa Roho Mmoja,” Wakorintho wa Kwanza 12, “sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, Roho Mtakatifu mmoja.” Kubatizwa kuwa Mwili mmoja, ambamo karama tisa za kiroho na ofisi nne za kiroho zimewekwa kwenye Mwili huo mmoja. Mle ndani, Mungu ameweka Kanisani, mitume, manabii, na kadhalika, katika Kanisa hili. Mle ndani kuna karama za uponyaji, miujiza, kunena kwa lugha, hekima, maarifa, hivyo hapo vitu ambavyo (ishara) vinamfuata mwaminio.

250 Mbona ukubali...Mbona ukubali...Kile nisichoweza kuelewa, ni kwa nini watu watake kupata magugu ya kale ya kielimu, wakati Mwamba umejaa asali. Jamani, kamwe siwezi kulielewa.

251 Na tuinamishe vichwa vyetu. Ungetaka kukumbukwa kwa maombi, ukisema, “Mungu nipe shauku ya moyo wangu. Ninampenda Bwana Yesu”?

252 Baba yetu wa Mbinguni, wakati mwingine baada ya ibada, nashangaa. Kwa nini Roho Mtakatifu sikuzote analipiga kanisa? Anafanyaje hilo? Hata hivyo, watu waliopakwa mafuta kwa Roho Mtakatifu hawawezi kusema yale wanayotaka kusema, inawabidi kusema asemayo Roho. Nasi tunaona kwamba katika Biblia ya Kale, mtwangaji dhahabu, mpigaji alipiga dhahabu, na kuipiga dhahabu, naye angeipindua na kuipigapiga mpaka uchafu ukaitoka; naye akaipiga kwa muda mrefu sana hata akaona uakisi wake mwenyewe katika hiyo dhahabu, ndipo akajua ilikuwa ni safi. Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu hulipigapiga kanisa, akalipindua, na kulihukumia *hili* na kulihukumia *lile,* mpaka anautoa uchafu wote, nao uakisi wa kweli wa Yesu Kristo unaakisi katika watu Wake; hata wana Uhai ule ule, ishara zile zile, wanafanya miujiza ile ile Yeye aliyofanya, uakisi wa Roho Mtakatifu katika hao watu.

253 Mungu, uchukue maskini moyo wangu. Nipigepige, nipindue, vyovyote utakavyo, Bwana, lakini hebu nimwakisi Yesu. Jalia nimwakisi Yeye, Bwana. Jalia watu wote hapa leo, Bwana, jalia sote tukuakisi Wewe; maisha Yako yenye upendo, utii Wako kwa Baba.

254 Ndio kwanza tuwaambie ya kwamba Wewe ulipungua katika umaarufu Wako. Ulipoenda kuwaponya wagonjwa, hakika, ulikuwa mashuhuri, watu walikuja kukuona Wewe. Lakini

ilikuwa ni nini? Mikate na samaki. Ndipo ulipowaambia Ukweli wa Neno, walikuwa hawataki kutembea katika Huo, ndipo umaarufu Wako ukaendelea kupunguka. Uliendelea mbele kufanya miujiza, lakini umaarufu Wako ukapungua.

255 Wewe ni Mungu wa uhalisi. Sikuzote umekuwa hivyo. Hubadiliki. Naomba, Baba, ya kwamba kanisa, na watu wote hapa walioinua mikono yao watapata ono la jambo hilo leo. Jalia waone, Bwana, ya kwamba sio mwanadamu. Kama tukimfuata mwanadamu, basi sisi ni wenye mashaka. Lakini kama tutamfuata tu Roho Mtakatifu, Yeye atatuongoza kwenye kila ahadi ya Biblia. Jalia kila kitu kitimizwe katika maisha ya watu hapa leo hii.

256 Nimeshika maskini nguo za watoto wachanga, majaketi, leso, vifurushi, mkononi mwangu. Tunafundishwa, katika Biblia, ya kwamba walichukua kutoka mwili wa Mtakatifu Paulo, leso na nguo; ndipo roho wachafu wakawatoka watu, na magonjwa yaliponywa. Watu siku hizi wangali wanamwona Mungu yeye yule. Sasa tunajua sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali ni Yesu. Wala haikuwa ni Mtakatifu Paulo; ilikuwa ni maisha ya Mtakatifu Paulo yaliyosalimishwa kwa Yesu Kristo. "Bwana alifanya miujiza maalum," sio Paulo; Bwana!

257 Sasa, Baba Mungu, tunaamini kwamba hatujui jambo moja, mara nyingi tunakosolewa; kutawadha miguu, kubatiza katika Jina la Yesu Kristo, kukataa wahubiri wanawake, kuamini katika usalama wa Milele wa nafsi, kama Paulo alivyofundisha. Akawaambia Waefeso, "Walichaguliwa tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wawe wana na binti za Mungu." Akawaambia Wakorintho ya kwamba, ya kwamba "Mungu alimchukia Esau na kumpenda Yakobo, kabla hata hawajazaliwa, kabla hawajawa na nafasi ya kujua mema na mabaya," kwa sababu ya uteuzi Wa—Wake tangu zamani. Kujua Kwake tangu zamani kulimfanya ajue. Na, Baba, kwa nini wanaanguka juu ya vitu kama hivyo, ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na ishara na maajabu kama vile Wewe ulivyoahidi, Biblia ikisema, "Wewe ni yule yule jana, na hata milele"? Baba, hatumaanishi kuwa tofauti. Lakini sisi... kwa...kusudi tuwe watumishi Wako, hatuna budi kulifuata Neno Lako. Naomba, Baba, kwamba Wewe utawajalia hawa watu waone ya kwamba sio kuwa tofauti ama kuwa wachoyo, ama kujaribu kuwa mtu fulani tusiye. Tunajaribu tu kulishikilia Neno Lako. Jalia kila mtu aone hilo, Baba.

258 Na ninapozituma nguo hizi kwa wagonjwa, jalia kila mmoja wao aponywe, Bwana. Jalia Roho Wako Mtakatifu aone onyesho hili la imani, na jalia waende wakaponywe. Tujalie, Bwana.

259 Mbariki Ndugu Neville. Libariki kanisa, pamoja. Bariki shule ya Jumapili, walimu. Wabariki wachungaji wote hapa. Wabariki wageni malangoni petu.

260 Bwana, unisaidie. Inanibidi kuendesha kwa kasi sasa, nipate kufika huko, nipate kuifariji familia iliyovunjika moyo; maili mia moja na hamsini, ama zaidi, huko chini mashambani, muda kidogo tu nipate kufaulu. Kuwa pamoja nami, Bwana. Nisaidie. Pia jalia katika hili . . . Kamwe, kamwe sipendi kuzungumza juu ya mtu aliyetuacha mpaka niwape wale, ambao wanasimama karibu, nafasi ya kukupokea Wewe. Mungu, jalia kwamba wengi tu wa maskini watu hawa wa Kentucky watapanda juu madhabahuni alasiri ya leo kwa unyenyekevu, katika kanisa hilo la Kimethodisti, na kuitoa mioyo yao Kwako. Tujalie, Bwana. Uturehemu sasa.

261 Tubariki, pamoja. Waponye walio wagonjwa, na uwaokoe waliopotea. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

262 Nitamwomba Ndugu Neville kuichukua ibada kwa dakika chache tu sasa, apate kuendelea, wala sijui yale atakayofanya kwenye wakati huu. Basi nyote mniombee, nami nitawaona baadaye. Mungu awabariki, Ndugu Neville.

60-0626 Kweli Zisizoshindwa Za Mungu Aliye Hai
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org